SportPesa
TZS. 576,086,780
BET LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Serikali** yamega hifadhi kuhalalisha mipaka ya vijiji 22

UKURASA 2



City yakomaa na Haaland

UKURASA 22

Nipashe
Ijumaa Oktoba 15, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580734
MWANGA WA
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Ma-RC na ma-DC wawekwa mtegoni

• **Ni** wale Mwenge uligundua madudu miradi ya maendeleo, sasa mikononi mwa Samia, TAKUKURU yatoa ripoti... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**WANAOISHI NA VVU WAOMBWA KUPATA CHANJO YA UVIKO-19**

WATU wanaoishi na virusi vya Ukimwi (VVU) Mkoa wa Njombe, wamehimizwa...

UKURASA WA 8

**TALGWU YATAKA HATUA MAUAJI YA MTENDAJI DAR**

CHAMA cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU) kimevitaka vyombo vya dola kuchukua hatua...

UKURASA WA 9

**MFANYABIASHARA APORWA FEDHA, ATWANGWA RISASI**

JESHI la Polisi mkoani Rukwa linawasaka watu wasiojulikana kwa tuhuma za kumjeruhi mfanyabiashara wa...



Rais na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Samia Suluhu Hassan, akipokea Mwenge wa Uhuru kutoka kwa Kiongozi wa mbio Maalum za Mwenge Kitaifa 2021, Luteni Josephine Mwambashi, baada ya kufikia kilele, katika Uwanja wa Magufuli, wilayani Chato, mkoani Geita jana. **PICHA: IKULU**

## Mwandishi The Guardian ang'ara tuzo Afrika

UKURASA 3



## Nyerere alivyoishtukia kasi ya kuzaliana nchini

UKURASA 14

MICHEZO YANGA YAJIWEKA MGUU SAWA BARA UK.24
MAONI, KATUNI UK.6



Meneja wa Mafunzo ya Usalama na Afya wa Kampuni ya TBL, Alberto Mramba (kushoto), akieleza kuhusu mchakato wa uzalishaji bia kwa askari wanafunzi kutoka Chuo cha Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) cha Babati, mkoani Arusha wakati walipotembelea kiwanda cha Ilala, jijini Dar es Salaam jana. PICHA: MPIGAPICHA WETU

# Samia awaweka mtegoni ma-RC, ma- DC

**Na Richard Makore,** CHATO

RAIS Samia Suluhu Hassan amewaweka mtegoni wakuu wa mikoa, wilaya na wakurugenzi wa halmashauri ambao maeneo yao yamebainika kuwa na miradi yenye harufu ya ufisadi.

Ameyasema hayo jana mjini hapa katika sherehe za kupokea na kuzima Mwenge wa Uhuru.

Awali, ilielezwa kuwa miradi 49 ya maendeleo 49 katika wilaya mbalimbali nchini yenye thamani ya Sh. bilioni 68.3, haikuzinduliwa wakati wa mbio za Uwenge wa Uhuru zilizohitimishwa jana.

Rais Samia alisema hajui imekuwaje mbio za Mwenge zibaini madudu hayo katika wilaya 38 nchini wakati kuna viongozi huko na kusisitiza kuwa hizo ni dalili mbaya kwamba viongozi hao hawafuatilii miradi mbalimbali ya serikali katika maeneo yao.

Kutokana na dalili hizo, Rais aliagiza kuwa kuwa fedha zilizotolewa hivi karibuni kwa ajili ya miradi mbalimbali zisiguswe na kuagiza viongozi katika maeneo hayo wazifuatilie. Hivi karibuni serikali ilipokea Sh. trilioni 1.3 kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwa jitihada za kuendeleza miradi na mapambano dhidi ya corona. Kuhusu vitendo vya rushwa, Rais Samia alivikemea kwa kuwa vinakwamisha maendeleo huku akiweka bayana kwamba rushwa inakwamisha uwekezaji nchini na kwamba inakwamisha juhudi za serikali kuwapelekea wananchi maendeleo.

**MIRADI UFISADI**

Awali, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu, Kazi, Vijana na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alisema miradi 49 ya maendeleo yenye thamani ya Sh. bilioni 68.3 haikuzinduliwa katika Mbio za Mwenge zilizohitiimishwa jana.

Mhagama alisema miradi hiyo haikuzinduliwa na kiongozi wa mbio za Mwenge baada ya kuitilia mashaka.

Kutokana na hali hiyo, alisema Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) iliagizwa kuichunguza na tayari ripoti yake jana ilikabidhiwa kwa Rais Samia kwa ajili ya hatua zaidi.

Uchunguzi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na (Rushwa), umebaini kulikuwapo na dosari katika miradi hiyo na kuomba kwamba mwakani Mwenge huo ukamulike miradi yote ambayo inafadhiliwa na serikali kupitia fedha zilizotolewa hivi karibuni na Rais Samia.

Licha ya miradi hiyo kukataliwa, Mhagama alisema miradi 1067 yenye thamani ya Sh. Trilioni 1.2 ilizinduliwa katika mbio hizo ikiwamo afya, mazingira, TEHAMA, fedha na utawala bora, elimu na maji.

Akizungumzia umuhimu wa Mwenge huo, alisema taifa limetimiza miaka 22 bila kuwapo Hayati Mwalimu Julius Nyerere ambaye alikuwa mwasisi wake na kwamba alikuwa mtetezi wa wanyonge.

Ujumbe wa mwaka huu wa Mwenge wa Uhuru ni "TEHAMA ni Msingi wa Taifa, Itumie kwa Usahiji na Uwajibikaji".

Kwa mwakani, alisema Mbio za Mwenge uzinduzi utafanyika mkoani Njombe na kilele chake ambacho huenda sambamba na Wiki ya Vijana kitakuwa mkoani Kagera.

**AMSIFU NYERERE**

Katika maadhimisho ya Kumbukumbu ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, alisema kiongozi huyo mwasisi wa taifa la Tanzania, alikuwa mtu anayeheshimu utu wa watu na kwamba alikuwa na uzalendo wa hali ya juu.

Alisema Nyerere aliunganisha taifa hili na kwamba serikali pamoja na wananchi wataendelea kumuenzi kwa vitendo.

Mwalimu Nyerere aliyoiongoza Tanganyika mwaka 1961 kupata uhuru kutoka kwa Waingereza na baadaye Tanzania baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964 hadi mwaka 1985, alifariki dunia Oktoba 14, 1999 katika Hospitali ya Mtakatifu Thomas, London, Uingereza alikokuwa akipatiwa matibabu.

Kutokana na kifo chake, Tanzania kila mwaka imekuwa ikiadhimisha siku hiyo kwa kumbukizi yake pamoja na shughuli mbalimbali zikiwamo za kitaaluma na midahalo kwenye taasisi za serikali na binafsi.

**MCHAKATO MKOA**

Katika hatua nyingine, Rais Samia aliweka kiporo suala la Chato kuwa mkoa huku akisema mchakato wa kufikia uamuzi bado unaendelea ikiwamo kukamilisha vigezo vinavyotakiwa ili kutangazwa mkoa huo.

Pamoja na hayo, Rais alisema miradi yote iliyoahidiwa na Hayati John Magufuli, Rais wa Awamu ya Tano, itakamilishwa kama ilivyopangwa. Aliitaja miradi hiyo kuwa ni pamoja na kukamilisha Hospitali ya Rufani ya Chato, Chuo cha VETA, bandari, uwanja wa ndege na msikiti.

# Serikali yamega ardhi hifadhi kuhalalisha mipaka ya vijiji 22

**Na Munir Shemweta,** UYUI

SERIKALI imetoa sehemu ya ardhi ya Hifadhi ya Mto Igombe kwa ajili ya wananchi wa vijiji 12 vilivyoko kwenye Wilaya ya Uyui mkoani Tabora.

Utoaji sehemu ya ardhi hiyo ni mwendelezo wa hatua ya Rais Samia Suluhu Hassan kuhakikisha anawabakisha wananchi walioingia kwenye mgogoro wa muda mrefu na serikali kwa kuvamia maeneo ya hifadhi za misitu, mapori ya akiba na pembezoni mwa maeneo chepechepe.

Baadhi ya vijiji vilivyonufaika na hatua hiyo ya serikali ni pamoja na vijiji vya Mbeya, Ishihimulwa, Gilimba, Nzubuka, Izugawima, Kingwanhoma, Usagali, Bukala pamoja na kijiji cha Uwimate

Kamati ya mawaziri wanane wa wizara za kisekta ikiwa wilayani Uyui juzi, baadhi ya wajumbe wake walitumia usafiri wa pikipiki kufika sehemu ya maeneo ya vijiji kikiwamo Ishihimulwa ili kutoa mrejesho wa utekelezaji uamuzi wa Baraza la Mawaziri kuhusu utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji.

Akiwa katika Kijiji cha Ishihimulwa, Mwenyekiti wa Kamati ya Mawaziri, William Lukuvi, ilibidi ahutubie wakazi wa eneo hilo akiwa kwenye helikopta baada ya wananchi kuamua kuufuata ujumbe wa mawaziri hao eneo ilipotua badala ya sehemu iliyopangwa kwa mkutano wa hadhara.

Aidha, kamati hiyo ilifika kijiji cha Kangeme wilayani Urambo ambako Lukuvi, ambaye ni Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, aliwaeleza wakazi wa eneo hilo kuwa mipaka ya hifadhi ya msitu wa Ulyankulu iheshimiwe na wananchi waendelee kusalia maeneo waliopo sasa.

"Pamoja na hifadhi ya msitu kusajiliwa mipaka yake iheshimiwe na wananchi mbaki maeneo yenu kama mlivyo na tutaiacha timu ifanye tathmini hapa na tathmini hiyo itakuwa shirikishi," alisema.

Mawaziri waliokuwa kwenye msafara huo, kila mmoja alielezea mipango ya serikali kuhusu utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi kwenye vijiji 975. Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alisema ni vyema wananchi wakaheshimu mipaka ya maeneo ya hifadhi na kuacha tabia ya kuvamia maeneo hayo kwa kuwa si ya kuchungia mifugo.

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, aliwaambia wananchi wa Urambo kuwa pamoja na Kamati ya Mawaziri kujikita kutafuta suluhu ya migogoro ya ardhi, serikali imesikia kilio cha muda mrefu cha tatizo la maji kwenye jimbo hilo na sasa watapelekewa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria.

Naibu mawaziri nao waligusia mikakati ya wizara zao kuhusu vijiji vilivyorasmishwa katika maeneo ya hifadhi akiwamo Mary Masanja wa Maliasili na Utalii, ambaye aliwahimiza wananchi kuhakikisha hawavamii tena hifadhi na waheshimu mipaka kwa kuacha kufanya shughuli zinazoweza kuharibu misitu.

Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Hamad Chande, aliwaambia wakazi wa vijiji hivyo kuwa utunzaji mazingira si suala la hiari kwa kuwa wananchi wanatakiwa kuyatunza na wasipofanya hivyo mazingira hayo yataharibu mfumo wa maisha.

Naye David Silinde, Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, alisema serikali mbali na kupeleka fedha za maendeleo kwenye tarafa na maeneo mbalimbali nchini haijalisahau Jimbo la Urambo ambapo kwa upande wa barabara, imetenga takriban Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya barabara za vijijini.

Mawaziri wa wizara za kisekta wamemaliza ziara kwenye mkoa wa Tabora ukiwa ni wa 4 tangu kuanza ziara yao ya kutembelea mikoa 10 na leo wanaendelea na ziara hiyo Mara kwa lengo la kupeleka mrejesho wa uamuzi wa baraza la mawaziri kuhusu utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975.

# Mwandishi The Guardian ang'ara Tuzo za FEMNET

**Na Mwandishi Wetu**

MWANDISHI wa habari wa magazeti ya The Guardian na Nipashe, Jenifer Gilla, ameshinda Tuzo ya Usawa wa Kijinsia, kipengele cha mazingira, zinazotolewa na Shirika la The African Development and Communication (FEMNET).

Tuzo hizo zilitolewa juzi mjini Nairobi nchini Kenya, katika hafla ya Mkutano Mkuu wa nane wa FEMNET wa kutetea haki za wanawake.

Tuzo hizo zilitolewa katika makundi matano ya kuzuia ukatili dhidi ya wanawake na mabinti likiwamo la mazingira, uongozi wa wanawake wenye mabadiliko, haki ya kiuchumi na haki ya afya ya uzazi.

Katika mashindano hayo jumla ya wanahabari 389 kutoka nchi 17 za Afrika na kati yao 15 walishinda katika mashindano hayo katika nafasi ya kwanza, pili na tatu.

Mratibu wa mkutano huo, kutoka FEMNET, Rachel Kagoiya, akizungumza kuhusiana na mkutano huo, alisema ulifanyika kwa siku mbili kuanzia Oktoba 12 hadi 14 na jumla ya washiriki 100 walikutana na wengine kwa njia ya mtandao kutokana na janga la UVIKO-19.

"Nafikiri wanachama kutoka Tanzania kikiwamo Chama cha Wanahabari Wanawake (TAMWA), wamefanya kazi ya kutetea haki za wanawake na wasichana kwa miaka 12 sasa," alisema.

Alisema walitoa tuzo hizo kwa mara ya kwanza ili kuwatambua waandishi wa habari wanaofanya kazi nzuri ya kuandika changamoto za wanawake.

Alisema mkutano huo ulitambulika kwa jina la Wanawake wa Kiafrika, Jinsia na Wanaharakati wa Haki za Wanawake wa Pan-African.



Mwandishi wa habari wa magazeti ya The Guardian na Nipashe, Jenifer Gilla (katikati), akiwa ameshika Tuzo ya Usawa wa Kijinsia, kipengele cha mazingira, iliyotolewa na Shirika la The African Development and Communication (FEMNET), baada ya kukabidhiwa katika hafla ya Mkutano Mkuu wa nane wa shirika hilo, jijini Nairobi, nchini Kenya, juzi. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji TAMWA, Rose Rueben, Kulia kwake ni Aurelia Gabriel, Mwandishi wa Gazeti la Mwananchi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanaoishi na VVU waombwa kupata chanjo ya Uviko-19

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WATU wanaoishi na virusi vya Ukimwi (VVU) Mkoa wa Njombe, wamehimizwa kujitokeza ili kupata chanjo ya Uviko-19 kwa kuwa wapo kwenye kundi hatarishi.

Wito huo umetolewa jana na Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Njombe, Kasanga Kasanga, wakati wa makabidhiano ya vifaa vya kujikinga na Uviko-19 pamoja na pikipiki kutoka Baraza la Taifa la Watu Wanaoishi na virusi vya Ukimwi Tanzania (NACOPHA).

"Usalama wetu kwenye hii Covid ndugu zangu tusikwepe kuchanja, tuache maneno ya mitaani kwamba tusichanje, twende tuchanje ili tuwe salama na sisi tuko katika hiari ukichanja una amani tujitambue katika mengi ikiwamo hili tusiwe na magonjwa mawili, mimi nishauri sisi tuwe namba moja kuchanja," alisema Kassanga.

Naye Meneja wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (NAKOPHA), Ferdinand Mazuni, alisema ipo haja ya kuhimizana suala zima la kuchanjwa ili kuwa salama.

"Naomba nisisitize hili suala la chanjo usipochanja madhara yake ni makubwa sana kwa hiyo kiongozi unapokwenda kwenye kikundi chochote, karani unapotembelea kikundi chochote wewe kama ni kiongozi wa kikundi chochote basi tuhimizane tuchanje kwa sababu madhara ya corona ni makubwa sana, ukiambukizwa uponaji wake ni mgumu sana, tukumbushane jamani," alisema Mazuni.

Mwenyekiti wa Konga Halmashauri ya Mji wa Njombe, Mary Mng'ong'o, alishukuru kutolewa kwa msaada huo kuwa unakwenda kutatua changamoto zilizokuwa zikiwakabili.


Canara Bank (Tanzania) Ltd.
(Together we can build a better life)

PUBLICATION OF INTEREST RATES, FEES AND CHARGES

PURSUANT TO REGULATION 40(3)(a) OF THE FINANCIAL CONSUMER PROTECTION 2019 AND REGULATION 11 OF THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS DISCLOSURE REGULATION, 2014.

| | TZS | USD |
|---|---|---|
| **A. SAVINGS BANK** | | |
| 1. Monthly Maintanance Charges | FREE | FREE |
| 2. Non Maintanance of Minimum Balance | FREE | FREE |
| 3. A/C Statement Charges | | |
| a) Monthly | FREE | FREE |
| b) Interm | 5,000.00 | $5 |
| 4. Cash Withdrawl Charges | FREE | Upto 5000 Free<br>Above 5000 - 0.3% |
| 5. Cash Deposit Charges | FREE | FREE |
| 6. Balance Confirmation certificate | 15,000.00 | $7 |
| 7. A/c Closure charges | 15,000.00 | $15 |
| 8. Activation of Dormat A/c | 6,000.00 | $6 |
| **B. CURRENT ACCOUNT** | | |
| 1. Monthly Maintanance Charges | FREE | FREE |
| 2. Non Maintanance of Minimum Balance | FREE | FREE |
| 3. A/C Statement Charges<br>a) Monthly<br>b) Interm | **5000<br>5000+500 for each page** | **$5<br>$ 5+1 for each page** |
| 4. Cash Withdrawl Charges | UPTO 25 MIO- FREE<br>ABOVE 25 MIO--0.12% | Upto 5000 Free<br>5000 to 10,000 - 0.3%<br>Above 10,000 - 0.5% |
| 5. Cash Deposit Charges | UPTO 50 MIO- FREE<br>ABOVE 50 MIO--0.12% | **Upto 10,000- Free<br>> 10,000- 0.3%** |
| 5. Balance Confirmation certificate | 25,000.00 | $15 |
| 6. Stop Payment Charges | 30,000.00 | $15 |
| 7. Cheque Return Charges | | |
| a) Inward | 30,000.00 | $15 |
| b) Outward | 30,000.00 | $20 |
| 8. A/c closure charges | 25,000.00 | $20 |
| **C. MOBILE BANKING CHARGES** | | |
| 1. Cash Withdrawal | | |
| Upto 100,000 | 2,000.00 | NA |
| 101,000 to 200,000 | 3,000.00 | NA |
| 201,000 to 400,000 | 5,000.00 | NA |
| 401,000 to 600,000 | 6,000.00 | NA |
| 601,000 to 999,000 | 8,000.00 | NA |
| **2. Funds Transfer/Mobile Wallet** | | |
| Upto 100,000 | 500.00 | NA |
| 101,000 to 250,000 | 1,000.00 | NA |
| 251,000 to 500,000 | 2,000.00 | NA |
| 501,000 to 1,000,000 | 5,000.00 | NA |
| 1,001,000 TO 10 Mn | 10,000.00 | NA |
| **Mobile Banking Services** | | |
| A) Monthly Subscription Charges | 500.00 | NA |
| B) PIN Request | 2,500.00 | NA |
| **H. LOCKERS RENT YEARLY** | | |
| 1.SMALL | 350,000.00 | |
| 2. MEDIUM | 600,000.00 | |
| 3. BIG | 750,000.00 | |

| D. REMITTANCES | TZS | USD |
|---|---|---|
| 1. TISS | 11,800.00 | $11.8 |
| 2. E Remittances | | |
| Upto USD 1000 or Eq. TZS | 20,000.00 | $10 |
| 1001 to 5000 | 24,000.00 | $12 |
| 5001 to 10000 | 48,000.00 | $25 |
| 10,001 and above | 100,000.00 | $50 |
| 3. SWIFT | | |
| a) Swift Outward | | |
| Upto 5,000 | NA | $45 |
| 5,001 to 10,000 | NA | $60 |
| above 10,000 | NA | $90 |
| b) Swift Inward | | |
| Upto 5,000 | NA | $12 |
| 5,001 to 10,000 | NA | $18 |
| above 10,000 | NA | $30 |
| **E. LOAN/ADVANCES RELATED CHARGES** | | |
| 1. Processing Charges | Upto 5 Mio - 25,000<br>5Mio to 10 Mio - 200,000<br>10 Mio to 25mio - 400,000<br>25 mn to 500 mio - 1.5%<br>>500mio--1.25%*<br>*minimum 7.5mio | Upto 5,000 - $100<br>5000 to 10,000 - $200<br>Upto 20,000 - $300<br>20,000 to 500,000 - 1.5%<br>>500,000--1.25%*<br>*minimum 7,500 |
| 2. Documentation Charges | Upto 100 mio --NIL--<br>>100 Mio 0.3% -Min 300,000 | Upto 50,000 --NIL--<br>>50,000 - 0.3% Min 150 |
| 3. Upfront fee on Term Loan | Upto 5Mio - 25,000<br>5 Mio to 10 Mio - 200,000<br>10Mio 25mio - 450,000<br>25 mn to 500 mio -1.8%<br>>500mio--1.5%*<br>*minimum 9mio | Upto 20,000 - $300<br>20,000 to 500,000 - 1.8%<br>>500,000--1.5%*<br>*minimum 9000 |
| 4. Inspection Charges | Upto 100 Mio -25,000<br>>100 mio - 50,000 | Upto 50,000 - 25<br>>50,000 ----50 |
| 5.Credit Reference Report Charges from D&B Tanzania | TZS 120,000 | USD 50 |
| 6.Pre-payment penalty | 2.00% of pre-paid amount in the case of takeover of liability by other bank/lenders | 2.00% of pre-paid amount in the case of takeover of liability by other bank/lenders |
| **F. LETTER OF CREDIT** | | |
| **Import Letter of Credit (per qrtr of Part thereof)** | | |
| Opening commission | NA | 1.2% ( Min $ 200) |
| LC amendment Commission | NA | 0.4% ( Min $50 max 350) |
| Swift charge for LC opening | NA | $40 |
| Swift charge for other message/amendments | NA | $40 |
| Extensions - Commissions | NA | 1.2% ( Min $200) |
| LC cancellation charges | NA | 1.2% ( Min $200) |
| Non payment of Bills on due date | NA | 16% Till Payment |
| **Export Letters of Credit (per quarter or part thereof)** | | |
| Advising commission | NA | $140 |
| Confirmation Commission | NA | 0.5% ( Min $150) |
| Negotiating bills under LC | NA | 0.5%(Min $75+cuourier+int) |
| Reimbursement claim paid | NA | 0.5% ( Min$75) |
| Extensions - Commissions | NA | 1.2% ( Min $200) |
| Collection of Export LC | NA | 0.5%(Min $75+cuourier+int) |
| Amendments | NA | $75 |
| **G. Guarantees (Local & International)** | | |
| Bonds & Guarantees | 1.2% ( Min TZS 75,000) | 1.20% |
| Bonds & Guarantees with 100 % Cash Margin | 0.5% per quarter (Min TZS 75,000) | 40% of actual charges |

**OTHER DISCLOSURES(VIAMBATANISHI)**

| | TZS | USD |
|---|---|---|
| 1. Base or Prime Lending Rate | 16 | 7 |
| 2. Maximum spread above Base or Prime Lending Rate | 5 | 5 |
| 3.Penal Interest | | |
| a. For non compliance on Terms of Saction | 3% p.a over regular rate of interest | |
| b. For Overdrawing/Excess drawing due to non payment of interest/installment/charges | 5% p.a over regular rate of interest | |
| 4. Deposit Rates | | |
| a. Current account | Nill | Nill |
| b. Savings bank deposit | 3.00% | 1.00% |
| c. Fixed deposits | | |

i. Fixed Deposits of TZS

| Amount in TZS | up to TZS 50 Million | Over TZS 50 Million up to 100 Million | Above 100 Million |
|---|---|---|---|
| 30 -90days | 3.50% | 4.50% | 5.50% |
| 91-180days | 4.50% | 5.50% | 6.50% |
| 181-364 days | 5.50% | 7.00% | 7.50% |
| Above 1 year | 8.00% | 8.25% | 8.50% |

ii. Fixed Deposits of USD

| Amount in USD | up to USD 50,000 | Over USD 50,000 up to USD 100,000 | Over USD 100,000 |
|---|---|---|---|
| 30 -90days | 1.50% | 2.25% | 2.50% |
| 91-180days | 2.00% | 2.75% | 3.25% |
| 181-364 days | 2.50% | 3.00% | 3.50% |
| Above 1 year | 3.00% | 3.50% | 4.00% |

| NAME | TITTLE | SIGNATURE | DATE |
|---|---|---|---|
| JOHN CHARLES | GM-OPERATIONS | SIGNED | 12-10-2021 |
| JOHNVIAN NYAMSISA | GM-TREASURY | SIGNED | 12-10-2021 |
| KAUSHENDRA TIWARI | GM-CREDIT | SIGNED | 12-10-2021 |

216513502

TANGAZO

# UNITED BANK FOR AFRICA (TANZANIA) LIMITED

UBA

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA 30.09.2021

Imetolewa chini ya kanuni ya 32 kifungu namba 3 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2006

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya 30-Sep-21 | Robo Mwaka ya 30-Jun-21 |
|---|---|---|---|
| | **A. MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 6,571 | 4,260 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 24,017 | 8,476 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 19,182 | 28,070 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 17,159 | 5,967 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | 0 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 31,026 | 46,300 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 66,148 | 71,445 |
| 12 | Mali Nyingine | 10,984 | 10,271 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 2,045 | 1,853 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **177,133** | **176,642** |
| | **B. DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 9,302 | 48,196 |
| 18 | Amana za Wateja | 119,254 | 85,136 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 12,802 | 8,263 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,968 | 1,314 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 1,175 | 1,814 |
| 27 | Dhima Nyingine | 4,978 | 4,811 |
| 28 | Madeni | - | - |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **149,479** | **149,535** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29)* | **27,655** | **27,108** |
| | **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 31,420 | 31,420 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 29,104 | 29,104 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (37,053) | (37,053) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 4,184 | 3,636 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **27,655** | **27,107** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 1,002,626 | 951,915 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 4,149 | 4,029 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 354 | 354 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 16% | 15% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 6.24% | 5.60% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 50% | 77% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 37% | 40% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 66% | 83% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 41% | 10% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 0% | 14% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI
### KWA ROBO MWAKA ULIOISHIA 30 SEPTEMBA 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 30-Sep-21 | Robo ya Mwaka linganishi 30-Jun-21 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-21 | Limbikizo la Mwaka linganishi 30-Sep-20 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 3,144 | 3,109 | 9,056 | 3,085 |
| 2 | Gharama za Riba | (1,223) | (1,040) | (3,027) | (759) |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **1,922** | **2,069** | **6,029** | **2,326** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | - | - | - | - |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **2,510** | **3,664** | **9,242** | **3,553** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 413 | 257 | 981 | 458 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 2,074 | 3,355 | 8,147 | 3,081 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 24 | 52 | 113 | 13 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(3,765)** | **(3,796)** | **(10,912)** | **(3,820)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (1,744) | (1,615) | (4,975) | (1,581) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (270) | (413) | (987) | (361) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (1,751) | (1,768) | (4,951) | (1,877) |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **667** | **1,937** | **4,359** | **2,059** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (120) | (28) | (175) | (56) |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **548** | **1,910** | **4,184** | **2,003** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **548** | **1,910** | **4,184** | **2,003** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 124 | 121 | 124 | 115 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 87 | 304 | 666 | 319 |
| 15 | **Idadi ya Matawi** | 7 | 6 | 7 | 4 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| | (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.31% | 1.08% | 2.37% | 1.32% |
| | (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 2.00% | 7.05% | 15.28% | 8.38% |
| | (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 66.58% | 56.04% | 59.64% | 57.55% |
| | (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 1.47% | 1.42% | 4.60% | 1.76% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA
### KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 SEPTEMBA 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka ya sasa 30-Sep-21 | Robo ya Mwaka linganishi 30-Jun-21 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-21 | Limbikizo la Mwaka linganishi 30-Sep-20 |
|---|---|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | **548** | **1,910** | **4,184** | **2,003** |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 456 | 276 | 456 | 121 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 5,298 | (3,599) | 5,298 | 4,313 |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (238) | 19,825 | (238) | (56,877) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 8,887 | 1,896 | 8,887 | 54,428 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 167 | 1,086 | 167 | (12) |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (713) | (2,657) | (713) | (190) |
| - Kodi Iliyolipwa | - | - | - | - |
| -Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **14,405** | **18,737** | **18,041** | **3,785** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (372) | (661) | (372) | (225) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(372)** | **(661)** | **(372)** | **(225)** |
| ***III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:*** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | 29,916 |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | **-** | **-** | **-** | **29,916** |
| IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu: | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **14,033** | **18,076** | **17,670** | **33,476** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | 104,214 | 86,138 | 86,138 | 74,812 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka | **118,247** | **104,214** | **103,808** | **108,288** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA 2021

(Kiasi kwa shilingi millioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la ziada ya jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mwaka wa sasa 2021 | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (37,053) | - | - | - | 23,471 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | 4,184 | - | - | - | 4,184 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Share issued | | | - | | - | | |
| Salio la mwisho wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (32,869) | - | - | - | 27,655 |
| Mwaka uliopita 2020 | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (40,498) | - | - | - | 20,026 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | 3,445 | - | - | - | 3,445 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Share issued | - | - | - | - | - | - | - |
| Salio la mwisho wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (37,053) | - | - | - | 23,471 |

| | Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1 | Kingsley Ulinfun<br>**Mkurugenzi Mtendaji** | Imesainiwa | 15th October 2021 |
| 2 | Chomete Hussein<br>**Mkuu wa Fedha** | Imesainiwa | 15th October 2021 |
| 3 | Joseph Ringa<br>**Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | Imesainiwa | 15th October 2021 |

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| | Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1 | Amb.Tuvako Manongi<br>**Mkurugenzi** | Imesainiwa | 15th October 2021 |
| 2 | Oliver Alawuba<br>**Mkurugenzi** | Imesainiwa | 15th October 2021 |

United Bank for Africa (T) Ltd is a subsidiary of United Bank for Africa Plc, a leading Pan African bank offering universal banking to more than 13 million customers in over 1000 branches and outlets in Africa , USA and Europe .

East & South Africa
- Tanzania
- Kenya
- Congo DRC
- Mozambique
- Uganda
- Zambia

Central Africa
- Cameroon
- Gabon
- Tchad
- Congo Brazzaville

West Africa
- Ghana,
- Benin
- Burkina Faso,
- Cote D'Ivoire (CDI)
- Liberia
- Sierra Leone
- Senegal
- Mali
- Guinea

Europe
- UK
- France

USA
- New York

216515402

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mchakato maoni uraia pacha ni habari njema

**SERIKALI** imesema inakamilisha mchakato wa kupitia maoni ya Watanzania wanaoishi nje (Diaspora), kuhusu kupewa hadhi maalumu itakayowawezesha kushiriki masuala mbalimbali ya maendeleo nchini.

Uraia pacha ni kilio cha muda mrefu cha Watanzania wanaoishi nje na kuwa na uraia wa nchi nyingine kutokana na kushindwa kupata baadhi ya haki kwenye nchi yao na kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania ukishakubali kuwa raia wa nchi nyingine basi unakuwa umeukana uraia wa nchi yako.

Licha ya kuwa walizaliwa, kukulia, kusoma, kuishi na kuwa na familia zao Tanzania, haki zote muhimu hupotea wanapopata uraia wa nchi nyingine na kila wanapokuja nchini wanakuja kama wageni licha ya kwamba asili yao ni nchini.

Aidha, kutokana na hali hiyo wameshindwa kufungua akaunti na kuweka fedha kwenye benki za nchini, jambo ambalo kwao ni kikwazo kikubwa, kumiliki ardhi au kama alipewa mgao wa mali za urithi au ardhi anapoteza umiliki wake.

Uamuzi wa serikali wa mchakato wa kupitia maoni yao kwa ajili ya hatua zaidi za kwenda bungeni kupitishwa kwa ajili ya utekelezaji unaleta matumaini ya uwezekano wa Watanzania hao kupata haki zao muhimu.

Tunapongeza uamuzi huo kwa kuwa kwa miaka mingi imekuwa hitaji la kila Mtanzania anayeishi nje, lakini imeshindikana kutekelezeka kwa sababu mbalimbali ambazo serikali imezieleza, na sasa imeona kuna umuhimu wa kuchambua maoni yao na kuyafanyia kazi. Zipo nchi zinaruhusu uraia wa nchi mbili na umekuwa ni wenye manufaa kwa nchi zinazoendelea kwa kuwa wananchi wenye uraia wa nchi nyingine wamewekeza na kufanya shughuli za maendeleo ambazo zimekuwa zenye manufaa kwa nchi zao za asili, wengine wamerudisha utaalamu nyumbani.

Tunaamini mafanikio yao ni ya Watanzania wote kwa kuwa kama wakiweka fedha kwenye benki za nchi yao ya asili zitazunguka ndani na kukuza uchumi wa nchi, kuongeza ajira na maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Pia, kukiwa na uhakika wa kupata haki yao ni rahisi kuleta wawekezaji wengi na wao kuwekeza nchini kwa kuwa wana kuwa na haki ya ardhi na mali nyingine watakazowekeza.

Wapo Watanzania wanaomiliki mali kwenye nchi mbalimbali ambazo kwa kiasi kikubwa zimenufaisha uchumi wa nchi hizo.

Kwa Mtanzania aliye na uraia wa nchi nyingine hana haki ya kupiga kura kwa kiongozi yeyote katika uchaguzi wowote unaofanyika nchini, bali anakuwa na haki ya kuchagua viongozi kwenye nchi ambayo amepata uraia.


Watanzania hawa ambao wamepoteza haki yao ya kuzaliwa kwa kuwa walipata uraia wa nchi nyingine miongoni mwao kuna wataalamu wa fani mbalimbali ambazo zingeweza kulisaidia taifa kwa kiasi kikubwa iwapo wangepewa nafasi ya kuwekeza nchini.

Iwapo wangewekeza maana yake utaalamu wao ungebaki nchini, ungerithishwa kwa Watanzania wengine na kusaidia kuboresha huduma mbalimbali za kijamii, kwa kuwa utaalamu walionao wakati mwingine hapa nchini haupo au umekosa watu wa kuonyesha kwa vitendo, na wakati mwingine kutumika gharama kubwa kumuita mtaalamu kutoka nje ya nchi.

Wakati wa Bunge Maalum la Katiba hoja ya uraia pacha iliibuka na katika Rasimu ya Katiba ya Tume ya Marekebisho ya Katiba chini ya uenyekiti wa Jaji Joseph Warioba, liliwekwa kama sehemu ya mapendekezo ya Watanzania wanavyotaka Katiba mpya iwe.

Aidha, Watanzania waishio nje ya nchi zaidi ya milioni mbili walisaini waraka maalum kwamba Watanzania hao wapate haki yao ya kupiga kura kwa kuwa wana haki ya kuzaliwa nchini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Unapotaja Tanzania ya Viwanda, mikono yake Baba wa Taifa imo

Na Sabato Kasika

**WAKATI** wa utawala wake, Baba wa Taifa Hayati Julius Kambarage Nyerere, alijitahidi kuhakikisha uchumi wa nchi unaimarika kwa kuanzisha mikakati mbalimbali itakayowezesha kufikia lengo alilokusudia.

Miongoni mwake, ni kuanzisha vituo vya utafiti wa mazao ya chakula na mazao ya biashara, kwa lengo la kukuza soko la bidhaa za kilimo ili kukuza viwanda ambavyo alivianzisha.

Karibu kila zao linalolimwa hapa nchini lilikuwa na kiwanda chake, kuanzia pamba, tumbaku, chai, korosho, katani, bila kusahau viwanda vya nguo, zana za kilimo na vingine vingi.

Aidha, katika harakati zake za kuinua uchumi, hakuishia hapo bali alianzisha vituo vya uzalishaji mifugo, huku akihakikisha kuwapo kwa usimamizi wa uchumi wa viwanda vya mazao mbalimbali yanayolimwa nchini.

Vilevile, dira hiyo inalenga kuifanya nchi kuwa yenye amani, kuondoa rushwa na kujenga uchumi imara, pia kuhakikisha kwamba mazingira ya uwekezaji nchini yanakuwa bora zaidi.

Rais huyo wa kwanza wa Tanzania, ndiye aliyekuza soko la bidhaa za kilimo na viwanda kwa kuanzisha vituo vya utafiti wa mazao ya chakula na ya biashara kwenye baadhi ya mikoa nchini.

Nyerere aliiendeleza Tanzania kwa uchumi wa viwanda, ambao sasa serikali iliyopo madarakani ina Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Tanzania, inalenga kuifikisha nchi kuwa ya viwanda ifikapo mwaka 2025.

Serikali ya sasa inakuja na dhamira ya kufufua baadhi ya fikra na baadhi ya vitendo vya Baba wa Taifa, kwa kuja na dira hiyo inayolenga kuifikisha Tanzania ya Viwanda ifikapo mwaka huo.

Ni hatua ya kufufua viwanda vilivyokufa, pia kujenga vingine vipya, ni wazi kwamba kile kilichoanzishwa na Rais huyo wa kwanza, kinaendelezwa, ili hatimaye kufikia ndoto alizozikusudia kwa nchi hii.

Baba wa Taifa alitamani Tanzania kuwa ya viwanda na hatua ya nchi ilionyesha uthubutu, matamanio ambayo bado yanaendelezwa na serikali iliyopo madarakani, hasa kutokana na ukweli kwamba miaka ya katikati, kuanzia 1986 viwanda vingi viliyumba na vingine kufa.

Nchi kuwa na viwanda vingi na vya aina mbalimbali, ni hatua inayoweza kusaidia kuepuka mtindo tegemezi wa kuagiza vitu kutoka nje ya nchi, ambavyo vinazalishwa na viwanda vya ndani, na ndivyo Baba wa Taifa alikusudia. Wakati huu wa Maadhimisho ya Miaka 22 ya kifo chake muasisi wa taifa, ni vyema kukumbuka mengi ambayo aliyafanya katika nyanja mbalimbali, kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii, ikiwamo sekta ya viwanda.

Aliamini kuwa sekta ya viwanda ni muhimu katika kuchangia pato la taifa na kutoa ajira kwa Watanzania wengi husus an, vijana na kufanya kazi katika viwanda vidogo na vya kati.

Sekta hiyo, pia ina wajibu wa kukuza viwanda ni pamoja na kuongeza ujuzi kwa vijana, ili walete mabadiliko ya kiuchumi na kuwa miongoni mwa nguzo muhimu za ukuaji uchumi kitaifa. Kwa kutambua hilo, serikali iliweka nguvu kubwa katika kufanikisha utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda, sambamba na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa 2020/21-2025.

Hatua hizo zinazochukuliwa na serikali, ni wazi zinamuenzi Baba wa Taifa, ambaye alitamani Tanzania, iwe na viwanda vya kutosha kuanzia vya nguo hadi vya kuchakata mazao yanayozalishwa nchini.

Kwa kuwa alihakikisha karibu kila zao linalolimwa nchini lilikuwa na kiwanda chake, kuanzia pamba, tumbaku, chai, korosho, katani, ninaamini hatua hiyo inaweza kufikiwa na serikali, kwani imekusudia kuwa nchi ya viwanda.

Si kuwa Tanzania ya Viwanda tu, bali hatua hiyo inakusudia kukuza soko la bidhaa za kilimo na viwanda, kwa ajili ya kuinua uchumi wa nchi ili kuwafanya Watanzania waondokane na umaskini. Tijitahidi, tutafika.

■ **Soma safari ya viwanda nchini, Uk. 12.**

# TANGAZO

EAST AFRICAN
**CRUDE OIL PIPELINE**

## OMBI LA KUONESHA NIA YA KUTOA HUDUMA ZA UCHAPISHAJI TAARIFA PAMOJA NA BIDHAA ZENYE CHAPA KATIKA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI. KUMBUKUMBU. 0010007126

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V, inaalika taasisi na kampuni zenye weledi na uzoefu katika Nyanja ya uchapishaji wa nyaraka za mawasiliano katika mifumo mbalimbali pamoja na kutoa huduma ya bidhaa zenye chapa (Large Scale Printing and Products Branding) katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania.

### MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA

KAMPUNI inahitaji huduma za kampuni ya mawasiliano kutoa usaidizi katika moja au huduma mbalimbali tajwa kulingana na mahitaji:

- Huduma ya uchapishaji taarifa za mawasiliano katika mifumo mbalimbali.
- Kutoa huduma ya bidhaa zenye chapa ikiwa ni pamoja na mbao za matangazo na masanduku ya maoni yenye chapa.

### VIGEZO MUHHIMU

Makampuni au mashirika yatakayoonesha nia, yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa uzoefu wa utendaji kazi bora pamoja na sampuli za kutekeleza kazi za usaidizi katika mawanda ya mawasiliano ya nia husika, kampuni au Taasisi inaweza kuonyesha nia kwa zabuni moja au zaidi kati ya zilizoorodheshwa hapo juu. Katika hatua hii, sampuli zote za kazi za mawasiliano zinatakiwa kuwasilishwa kupitia uzi wa taarifa (link) ambao hautarajii kuisha muda wake.
- Uthibitisho wa uwezo mfano kuwa na vifaa, miundo mbinu pamoja na muundo wa timu ya watendaji.
- Uthibitisho wa kufanya kazi katika miradi mikubwa yenye uhitaji mkubwa wa usaidizi wa mawasiliano.
- Uthibitisho wa uzoefu na/au uwezo wa kusambaza na kubandika taarifa za mawasiliano katika ukanda wa kati katika mikoa ya Kagera, Geita, Tabora, Shinyanga, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga ikihitajika.
- Uwezo wa kifedha kuweza kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha mahesabu ya fedha ya mwaka 2020.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia ya kutoa usaidizi husika.
- Uzingatiaji wa Kanuni za Maudhui ya Wazawa za mwaka 2012 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Wazawa (Nafasi za Ajira na Huduma kwa Watanzania).
- Usajili stahiki kutoka kwa mamlaka za nchi zinazohusika kwa ajili ya kutoa huduma stahiki inapobidi.
- Uthibitisho wa usajili katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na Cheti cha Mwaka wa Karibuni cha Malipo ya Kodi.

Mashirika yenye nia ya kuleta maombi na ambayo yana uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu yanapaswa kueleza nia yao pamoja na kuambatanisha pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20 Mb) saa au kabla ya saa **11 jioni** za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **19 Octoba 2021. Kichwa cha Baruapepe: Kumbukumbu namba husika.**

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na mashirika yatakayoonesha nia ili kutengeneza orodha ya Mashirika ya awali yenye vigezo vinavyotakiwa. Mashirika yatakayokidhi vigezo tu ndiyo yatapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni. Maelezo yote ya kuonesha nia yanapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

EAST AFRICAN
**CRUDE OIL PIPELINE**

## OMBI LA KUONESHA NIA YA KUTOA HUDUMA ZA USAIDIZI KATIKA KITENGO CHA MAWASILIANO KATIKA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI. KUMBUKUMBU. 0010007127

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V, inaalika taasisi na kampuni zenye weledi na uzoefu katika Nyanja ya mawasiliano kuonesha nia ya kutoa huduma zinazohusiana na mawasiliano kwa Umma katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania.

### MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA

KAMPUNI inahitaji huduma za kampuni ya mawasiliano kutoa usaidizi katika moja au huduma mbalimbali tajwa kulingana na mahitaji:

- Sanaa ya kusanifu michoro, picha, miundo na alama kwa kutumia technolojia ya komputa (Graphics designing)
- Sanaa ya kusanifu miundo, picha na alama zenye mwendo, michoro yenye mwendo mfumo wa 2D &3D pamoja na michoro ya vielelezo kwa kutumia teknolojia ya komputa.
- Sanaa za jukwaani haswa katika maeneo ya mkuza wa bomba: Kagera, Geita,Tabora, Shinyanga, Singida, Dodoma, Manyara and Tanga.
- Huduma ya Kurekodi video zenye viwango vya juu pamoja na kuzihariri.
- Huduma za upigaji picha pamoja na uhariri wa picha.
- Huduma za kurekodi sauti ikiwemo kuzihariri.
- Tafsiri kutoka lugha ya Kiswahili kwenda Kiingereza na Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili hasa katika mfumo wa maandishi.

### VIGEZO MUHIMU:

Makampuni au mashirika yatakayoonesha nia, yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa uzoefu wa utendaji kazi bora pamoja na sampuli za kutekeleza kazi za usaidizi katika mawanda ya mawasiliano ya nia husika, kampuni au Taasisi inaweza kuonyesha nia kwa zabuni moja au zaidi kati ya zilizoorodheshwa hapo juu. Katika hatua hii, sampuli zote za kazi za mawasiliano zinatakiwa kuwasilishwa kupitia uzi wa taarifa (link) ambao hautarajii kuisha muda wake.
- Uthibitisho wa uwezo mfano kuwa na vifaa, miundo mbinu pamoja na muundo wa timu ya watendaji.
- Uthibitisho wa kufanya kazi katika miradi mikubwa yenye uhitaji mkubwa wa usaidizi wa mawasiliano.
- Uthibitisho wa uzoefu wa kufanya kazi katika ngazi za chini katika ukanda wa kati katika mikoa ya Kagera, Geita, Tabora, Shinyanga, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga Sanaa za majukwaani utapewa kipaumbele.
- Uwezo wa kifedha kuweza kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha mahesabu ya fedha ya mwaka 2020.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia ya kutoa usaidizi husika.
- Uzingatiaji wa Kanuni za Maudhui ya Wazawa za mwaka 2012 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Wazawa (Nafasi za Ajira na Huduma kwa Watanzania).
- Usajili stahiki kutoka kwa mamlaka za nchi zinazohusika kwa ajili ya kutoa huduma stahiki inapobidi.
- Uthibitisho wa usajili katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na Cheti cha Mwaka wa Karibuni cha Malipo ya Kodi.

Mashirika yenye nia ya kuleta maombi na ambayo yana uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu yanapaswa kueleza nia yao pamoja na kuambatanisha pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) saa au kabla ya saa **11 jioni** za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **19 Octoba 2021. Kichwa cha Baruapepe ni Kumbukumbu namba husika.**

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na mashirika yatakayoonesha nia ili kutengeneza orodha ya Mashirika ya awali yenye vigezo vinavyotakiwa. Mashirika yatakayokidhi vigezo tu ndiyo yatapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni. Maelezo yote ya kuonesha nia yanapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

# Airtel Money yatangaza gawio la bilioni 2.1/-

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Airtel Tanzania kupitia huduma yake ya Airtel Money imetangaza kutoa faida ya Sh. bilioni 2.1 kwa wateja na mawakala kuanzia jana.

Faida hiyo ni kwa kipindi cha robo mwaka ya kuanzia Aprili hadi Juni, mwaka huu na kwamba kwa kutumia gawio la faida mteja analopata kulipia huduma au bili mbalimbali atakavyo.

Mkurugenzi wa Airtel Money, Isack Nchunda, alisema jana kuwa: "Tunayo furaha siku ya leo tena kwa kutoa faida kwa wateja pamoja na mawakala wetu huku tukishuhudia huduma yetu ya Airtel Money ikikua siku hadi siku. Leo (jana) Airtel Money inatangaza kutoa faida ya Sh. bilioni 2.1 kwa wateja pamoja na Mawakala wa Airtel Money.

"Kila mteja na wakala atapata faida kulingana na matumizi yake ya huduma ya Airtel Money kwa kipindi cha robo mwaka kuanzia Aprili hadi Juni, 2021," alisema.

Alisema nia ya Aitrel ni kuendelea kuunga mkono juhudi za serikali kwenye suluhisho la kifedha nchini na kwamba faida wanayopokea wateja pamoja na mawakala ni kutokana na matumizi ya huduma yetu ya Airtel Money.

"Nachukua fursa hii kuwaomba Watanzania waendelee kutumia huduma ya kampuni yao ya Aitel kupitia huduma ya Airtel Money kwani inapatikana kwa urahisi, nafuu na salama," alisema Nchunda.

Meneja Uhusianao wa Airtel, Jackson Mmbando, alisema Airtel imedhamiria kuendelea kutoa huduma bora za Airtel Money pamoja na kusogeza huduma karibu na wateja, hivyo kuwafikia wengi ambao hawajafikiwa na huduma za kibenki.

Kwenye suala la kuwa suluhisho la kifedha hapa nchini, alisema Airtel hivi karibuni ilizindua huduma ya TUMA PESA BURE, ambayo inawapa fursa wateja wa Airtel Money kutuma pesa bure Airtel kwenda Airtel.

Airtel money ni huduma ya kufanya malipo kidigitali na imekuwa ikibuni huduma mara kwa mara kwa lengo la kutoa huduma bora na nafuu kwa Watanzania wote.

Tayari Money imeunganishwa na huduma za 1,000 za malipo zikiwamo malipo ya bili pamoja na huduma za malipo ya serikali huku pia ikiwa imeunganisha na zaidi ya benki 40 nchini ili kuwezesha malipo na uhamishaji wa miamala kuwa rahisi wakati wowote.

# RC: Wananchi changamkieni kampeni elimu kwa mlipakodi

**Na Mwandishi Wetu, SONGEA**

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Balozi Wilbert Ibuge, amewataka wananchi kuchangamkia kampeni ya elimu kwa mlipakodi ili kuongezea uelewa na uhiari wa kulipa kodi nchini.

Akizungumza na timu ya maofisa kutoka Mamlaka ya Mapato (TRA) Makao Makuu Dar es Salaam walipomtembelea ofisini kwake mkoani Ruvuma kumtaarifu kuhusu kuanza kwa kampeni hiyo, mkuu wa mkoa huyo alisema kuwa huu ni muda mwafaka wa walipakodi kuongeza uelewa wa masuala ya kodi ikiwa ni pamoja na kueleza vikwazo vinavyowakabili kwa lengo la kuzitafutia ufumbuzi.

"Nimefurahia ujio wa kampeni hii hapa mkoani kwangu, hivyo ninapenda kuwahimiza walipakodi wote kutoa ushirikiano kwa maofisa wa TRA wanaofanya zoezi hili ili waweze kujiongezea uelewa wa kodi, lakini ni wakati mwafaka wa kueleza changamoto zinazowakabili ili ziweze kutatuliwa na hatimaye kuongeza uhiari wa kulipa kodi," alisema.

Meneja wa Huduma kwa Mlipakodi kutoka TRA Makao Makuu, Honester Ndunguru, alisema lengo la kampeni hiyo ni kusogeza huduma karibu, kuwaelimisha walipakodi na kujenga urafiki kati ya TRA na walipakodi kwa ajili ya kuongeza ridhaa ya ulipaji kodi.

"Pamoja na kusikiliza kero na changamoto zinazowakabili walipakodi wetu, kampeni hii pia imelenga kutoa elimu, kusogeza huduma karibu kwa wateja wetu pamoja na kusajili walipakodi wapya ili kuongeza idadi ya walipakodi nchini na ridhaa ya kulipa kodi," alisema.

Mfanyabiashara wa duka la nguo mkoani hapa, Joseph Ngocho, baada ya kupata elimu ya kodi wakati wa kampeni hiyo, alisema ni mara ya kwanza maofisa kutoka makao makuu kumtembelea ofisini kwake na kumwelimisha kuhusu umuhimu wa kulipa kodi, hivyo ameomba utoaji wa elimu hiyo uwe endelevu.

Hekima Kaduma, mfanyabiashara wa duka la pembejeo, alisema kampeni ya elimu kwa mlipakodi pamoja na kuwapatia elimu ya kodi, pia inasaidia kuondoa hofu ya kuwaogopa maofisa wa TRA maana walipakodi wanapata muda wa kuzungumza na kubainisha vikwazo vyao.

"Kwa kweli ninaishukuru TRA kwa kutuletea kampeni hii maana inatupa muda wa kutosha wa kuelimishwa na sisi tunapata nafasi ya kutoa maoni na kero zetu tofauti na kusubiri kuwafuata ofisini ambapo unakuta wateja wengi lakini pia wakati mwingine tunapata woga wa kutoa dukuduku letu," alisema.

Kampeni ya elimu kwa mlipakodi mkoani Ruvuma ilianza Oktoba 13, mwaka huu, na inatarajiwa kumalizika Oktoba 27, 2021 ikipita katika wilaya zote za mkoa huo ambazo ni Namtumbo, Mbinga, Songea, Nyasa na Tunduru.



Ofisa Msimamizi wa Kodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Makao Makuu, Godfrey Kumwembe (kulia), akimwelimisha mfanyabiashara wa duka la pembejeo, Hekima Kaduma, kuhusu utumiaji sahihi wa mashine za EFD wakati wa kampeni ya elimu kwa mliapakodi inayoendelea mkoani Ruvuma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TALGWU yataka hatua mauaji ya mtendaji Dar

**Na Mary Geofrey**

CHAMA cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU) kimevitaka vyombo vya dola kuchukua hatua za kisheria, ikiwamo kuwakamata wale wote waliohusika na mauaji ya Ofisa Mtendaji wa Mtaa wa Msumi, Kata ya Mbezi, Manispaa ya Ubungo, Kelvin Mowo.

Vilevile TALGWU imesema tukio hilo huenda likawapa hofu watumishi wa kada hiyo ambao wanashughulika na kero za wananchi kuwa mazingira ya kufanyia kazi siyo salama.

Tamko hilo limetolewa juzi na Katibu Mkuu wa TALGWU, Rashid Mtima, katika taarifa yake kwa vyombo vya habari la kukemea kitendo hicho.

"Tunaviomba vyombo vya dola mara baada ya uchunguzi kukamilika wahusika wote wakamatwe haraka na kuchukuliwa hatua za kisheria ili iwe funzo na kukomesha kabisa vitendo hivyo viovu na vya kinyama kwani vinarudisha nyuma jitihada za serikali katika kutoa huduma kwa wananchi, kudumisha amani na kukuza uchumi wa nchi yetu," alisema Mtima.

Alisema kitendo cha mwanachama mwenzao kuuliwa akiwa kazini, kinaweza kusababisha maofisa watendaji kukata tamaa, kuvunjika moyo, kukosa ari na morali ya kufanya kazi.

"TALGWU inalaani vikali mauaji yaliyofanywa dhidi ya mwanachama wetu Mowo. Kitendo hiki hakikubaliki, ni kinyume cha sheria za nchi, haki za binadamu na wala siyo utamaduni wa Watanzania.

"Ikumbukwe kwamba maofisa watendaji ndio watumishi wa umma wanaofanya kazi kwa karibu kabisa na wananchi kwa kusikiliza kero na changamoto zinazowakabili na kuzipatia ufumbuzi, hivyo kwa tukio hili litafifisha ari ya utendaji kazi wao," alisema Mtima.

Aliwataka waajiri ambao wana jukumu la ulinzi na usalama wa wafanyakazi wake, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na halmashauri zote nchini, wahakikishe kunakuwa na mazingira salama kwa watumishi wa kada ya maofisa watendaji wakati wote wanapotekeleza majukumu yao.

Alisema TALGWU imeendelea kushirikiana na familia ya marehemu, menejimenti ya Manispaa ya Ubungo pamoja na watumishi wote wa Mkoa wa Dar es Salaam ili kuhakikisha taratibu zinazingatiwa katika hatua ya uchunguzi na mazishi ya mwanachama wao.

Mtima aliwahakikishia wanachama wote kuwa chama hicho kitaendelea kuhakikisha watumishi wote wa umma wanafanya kazi katika mazingira salama na ya amani kwa kipindi chote wanapotekeleza majukumu yao.

Mowo aliuawa Jumatatu ya wiki hii na watu wasiyojulikana baada ya kumvamia akiwa ofisini kwake Mtaa wa Msumi, Manispaa ya Ubungo mkoani hapa.

Maziko ya mtumishi huo yalifanyika jana katika makaburi ya Kondo yaliyoko Ununio Bahari Beach wilayani Kinondoni.

**HABARI KITAIFA**

# Mfanyabiashara aporwa fedha, atwangwa risasi

**Na Gurian Adolf,**
SUMBAWANGA

JESHI la Polisi mkoani Rukwa linawasaka watu wasiojulikana kwa tuhuma za kumjeruhi mfanyabiashara wa mjini hapa kwa risasi kisha kumpora fedha na simu za mkononi.

Kamanda wa Polisi mkoani humo, William Mwampaghale, amemtaja mfanyabiashara aliyejeruhiwa kuwa ni Exsavery Msigwa, anayeshughulisha na biashara ya wakala wa fedha kwenye mitandao ya simu.

Kwa mujibu wa Kamanda Mwampaghale, tukio hilo lilitokea Oktoba 12, majira ya saa 2:30 asubuhi wakati mfanyabiashara huyo akiwa anapanda gari lake kwa ajili ya kwenda kufungua sehemu ya biashara yake.

Alisema baada ya Msigwa kufungua mlango wa gari lake alivamiwa na watu hao waliomtaka awabakidhi begi dogo alilokuwa nalo ambalo lilikuwa na fedha na simu anazotumia kwenye biashara yake.

Kamanda alisema mfanyabiashara huyo alikataa kutoa begi hilo, ndipo alipopigwa risasi kwenye goti la mguu wa kulia na kisha kumnyang'anya begi hilo na funguo ya gari na kuondoka nalo na kumuacha akipiga kelele za kuomba msaada ambao hakuupata kutokana na wananchi kuhofia usalama wao.

Alisema majambazi hao waliendа kulitelekeza gari hilo na kuondoka na begi la hela pamoja na simu walizochukua kwa mfanyabiashara huyo.

Kamanda Mwampaghale alisema kuwa polisi inawasaka watuhumiwa wa tukio hilo ili wafikishwe mahakamani kujibu tuhuma zinazo wakabili.

## Diwani mstaafu aisaidia shule

**Na Halfani Chusi**

DIWANI mstaafu, Kuluthum Sagamiko, ametoa msaada wa mifagio 100 na majaba ya kuhifadhi taka katika Shule ya Upili Oysterbay mkoani Dar es Salaam ili kukabiliana na uhaba wa vifaa vya usafi shuleni huko.

Alisema amelazimika kutoa vifaa hivyo vyenye thamani ya Sh. 500,000 baada ya kuzuru shuleni huko na kubaini inakabiliwa na kikwazo hicho cha uhaba wa vifaa hivyo.

Akizungumza mbele ya wanafunzi wakati wa kukabidhi vifaa hivyo, Kuluthum ambaye kwa sasa ni mjumbe Kamati ya Utekelezaji Wilaya ya Kinondoni, alisema ametoa vifaa hivyo ili kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan katika mikakati yake ya kuboresha sekta ya elimu.

"Sote tunajua mama ameweka kipaumbele katika sekta ya elimu, hivyo kila mtu ana jukumu la kuunga mkono juhudi za mama kwa namna yoyote ile, mradi ajikite zaidi katika jambo la msingi.

"Kama mnavyojua, mama 'anaupiga mwingi' na mimi nimeamua kumuunga mkono kwa vitendo," Kuluthum alisema huku akishangiliwa na wanafunzi na walimu wa shule hiyo.

Aliwaomba wadau wengine kuunga mkono kwa matendo juhudi mbalimbali zinazofanywa na Rais Samia kwa maendeleo ya taifa.

"Katika awamu hii mama ameanzisha miradi mingi, hivyo wadau na watu mbalimbali tujitoe kwa moyo na tuunge mkono juhudi hizo kwa matendo. Kwa kufanya hivyo, kutasaidia taifa liweze kusonga mbele," alisema.

Mkuu wa Shule hiyo, Dicksoni Kajuna, alimshukuru diwani mstaafu huyo kwa kutoa msaada wa vifaa hivyo na kubainisha kuwa vitakwenda kusaidia katika usafi shuleni kwake.

"Niseme tu ukweli kwamba tumefurahi kwa kupewa msaada huu, ni ukweli usiopingika tulikuwa na uhitaji wa vifaa vya kufanyia usafi shuleni hapa, tunashukuru sana na shukurani hizi sio peke yangu, ni kwa niaba ya shule nzima," alisifu.




Meneja wa Baraza la Taifa la Watu wanaoishi naVirusi vya UKIMWI Tanzania (NACOPHA) Kanda ya Dar es Salaam, Victoria Humburya (wapili kulia), akikabidhi maboksi 20 ya taulo za kike kwa Mkuu wa Shule ya Sekondari Kibiti, Estomic Kimwemwe (kushoto), yaliyotolewa na baraza hilo kwa kuwezeshwa na Shirika la UNAIDS, kwa ajili ya wanafunzi wa kike zaidi ya 500 shuleni hapo, wilayani Kibiti, mkoani Pwani juzi. Kulia ni Ofisa Maendeleo wa wilaya hiyo, Anthony Nyange. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watalii 'Sauzi' watembelea Hifadhi ya Taifa ya Nyerere

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

JITIHADA za Rais Samia Suluhu Hassan za kuhamasisha utalii nje ya nchi zimeanza kuzaa matunda baada ya treni yenye mabewa 15 iliyobeba watalii kutoka Afrika Kusini, maarufu Sauzi, kuwasili katika Hifadhi ya Taifa ya Mwalimu Nyerere mkoani Morogoro.

Treni hiyo ambayo iliwasili juzi katika Stesheni ya Fuga iliyopo ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Mwalimu Nyerere, watalii hao wakiambatana na wasaidizi wao kwa ajili ya kutembelea hifadhi hiyo.

Akizungumzia ujio huo wa watalii hao, Ofisa Uhifadhi Mwandamizi, Hifadhi ya Taifa ya Nyerere wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Seth Mihayo, alisema ujio wao umetokana na hamasa inayoendelea kufanywa na Rais Samia kutokana na vivutio vilivyopo nchini ikiwamo hifadhi hiyo iliyopewa jina la Baba wa Taifa.

Alisema hifadhi hiyo kwa sasa ndio kubwa kuliko zote katika Bara la Afrika na ilipewa jina hilo ili kumuenzi Baba wa Taifa kwa kuwa ndio alikuwa mhifadhi wa kwanza na ina vivutio vingi vya wanyama.

Mhifadhi huyo alisema treni hiyo ya kwanza imekuja tangu kupungua kwa ugonjwa wa Uviko-19 na kwamba kabla ya ugonjwa huo, walikuwa wakipokea wageni wengi wa ndani na nje.

"Wageni wengi wanaofika katika hifadhi yetu wanaanzia Visiwa vya Zanzibar kwenye utalii wa fukwe na baadaye kuja kwetu kuangalia wanyama," alisema.

Alisema ujio wa watalii hao kutoka Afrika Kusini ni kielelezo cha ongezeko la watalii wengine kufika nchini kutokana na ahadi ya watalii hao kufikisha ujumbe nchini mwao baada ya kushuhudia vivutio hivyo na kupungua kwa ugonjwa wa Uviko-19.

Seth alisema hifadhini humo mna fursa mbalimbali katika kuwekeza upande wa utalii na kuwataka wenye uwezo kufika kwa ajili ya kuwekeza.

Kamishna Mwandamizi wa Uhifadhi Kanda ya Mashariki wa TANAPA, Zainabu Ally, alisema hifadhi hiyo imetokana na sehemu iliyokuwa Pori la Akiba Selous na imekuwa na vivutio vingi kulinganisha na hifadhi zingine nchini.

Mhifadhi wa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, Charles Mpeka, alisema kupokewa kwa watalii hao ni mwendelezo wa makundi ya wageni kutoka Afrika Kusini ambao wamekuwa wakivutiwa kutembelea hifadhi hiyo.

"Kuja kwa wageni hao ni mwendelezo wa wageni ambao wanaingia kwa ajili ya kuenzi Siku ya Mwalimu Nyerere," alisema Mpeka.

Mwongoza Watalii, Khalifan Kaswila, alihamasisha Watanzania kutembelea hifadhi hiyo na zingine nchini ili kujifunza mambo mbalimbali pamoja na kuona wanyama, ndege na vivutio vingine.

# Masharti magumu usajili vijiji yaja

**Munir Shemweta,**
TABORA

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, amesema kuanzia sasa hakuna kijiji kitakachosajiliwa bila kushirikisha wadau muhimu ili kuondokana na migogoro ya ardhi.

Hatua hiyo ni kutaka kuondoa mgongano uliojitokeza wakati wa kushughulikia migogoro ya matumizi ya ardhi kwenye vijiji 975 baada ya kubainika kuwa baadhi ya vijiji kusajiliwa ndani ya mipaka ya hifadhi.

"Rais Samia Suluhu Hassan ameelekeza TAMISEMI iwe inashirikisha wadau muhimu wakati wa kusajili vijiji ili kuondokana na migogoro ya matumizi ya ardhi iliyojitokeza kwenye vijiji 975," alisema Silinde juzi mjini hapa.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri, wakati Kamati ya Mawaziri nane ikishughulikia migogoro ya matumizi ya ardhi, baadhi ya vijiji vimeonekana kuwa ndani ya hifadhi na wananchi wake wamekuwa wakishiriki uchaguzi ukiwamo ule wa serikali za mitaa.

Wadau muhimu watakaoshirikishwa katika usajili wa vijiji ni pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii.

"Ofisi ya Rais TAMISEMI ndiyo inayohusika na usajili wa vijiji, lakini kutokana na matatizo yaliyojitokeza kwenye migogoro hii ya vijiji 975, kuanzia sasa hatutasajili tena kijiji mpaka tuwasiliane na sekta na wizara zingine," alisema.

Silinde alisema kutoshirikisha wadau muhimu wakati wa kusajili vijiji, kumesababisha kuwapo vijiji ndani ya maeneo ya hifadhi, hivyo kuchangia migogoro ya matumizi ya ardhi.

Wakati wa kushughulikia migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975 Kamati ya Mawaziri inayoongozwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ilibaini baadhi ya vijiji kusajiliwa ndani ya mipaka ya hifadhi na kuwa na miundombinu ya kijamii.

Akielezea utekelezaji wa uamuzi ya Baraza la Mawaziri kuhusu utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi kwenye vijiji 975, Waziri Lukuvi alisema mkoa wa Tabora unahusisha vijiji 100 na ni mkoa wenye vijiji vingi kulinganisha na mikoa mingine. Alisema vijiji 94 kati ya hivyo ndivyo vitakavyobaki na maeneo yake kama yalivyo.

Kwa mujibu wa Lukuvi, mchanganuo wa utekelezaji uamuzi wa Baraza la Mawaziri ni kuwa vijiji 50 vilivyosajiliwa ndani ya hifadhi vitaendelea na hadhi yake huku vijiji 15 migogoro yake ikiwa tayari imetatuliwa na kijiji kimoja vitongoji vyake vitabaki kwenye hifadhi.

Aidha, alisema kuna vijiji 11 vitakavyomegewa maeneo katika hifadhi na vijiji 17 vilivyokuwa na migogoro ya mipaka na hifadhi vitabaki lakini mipaka yake itarejewa kwa njia shirikishi.

"Rais Samia Suluhu Hassan ametuelekeza tutekeleze uamuzi huu kwa umakini mkubwa bila ya kuleta taharuki kwa wananchi na kwa kuzingatia maslahi mapana ya wananchi na taifa kwa ujumla," alisema Lukuvi.



Naibu Waziri wa Madini, Prof. Shukrani Manya (kulia), Rais na Mtendaji Mkuu wa Barrick, Mark Bristow (katikati) na Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, wakivuta pazia kuzindua maabara ya kisasa na ya kwanza barani Afrika ya kupima kiwango cha madini kwenye sampuli inayotumia teknolojia ya X-ray, katika Mgodi wa dhahabu wa Bulyanhulu, wilayani Kahama, mkoani Shinyanga.
**PICHA: JOHN BADI**

# Serikali yatia saini hati ya uwekezaji

**Na Mary Geofrey**

SERIKALI imetia saini hati ya ushirikiano wa uwekezaji na Jumuiya ya Muungano wa Wafanyabiashara wa Kimataifa chini ya Kundi la Afrika na Asia (AFASU) katika sekta za utalii, kilimo, afya, elimu na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji, Geoffrey Mwambe, alitia saini makubaliano hayo na wajumbe wa jumuiya hiyo juzi mkoani Dar es Salaam kwa niaba ya serikali.

Mwambe alisema serikali imeweka mazingira wezeshi yanayovutia wawekezaji kuja kuwekeza nchini na kwamba ofisi yake itaratibu shughuli za uwekezaji wanaokusudia kuufanya nchini.

Alifafanua kuwa wawekezaji hao ambao ni Jumuiya ya Wafanyabiashara ambao wana kampuni binafsi watashirikiana na Tanzania katika sekta mbalimbali kwa lengo la kukuza uchumi wa taifa.

"Wanataka kufanya utalii nchini kila mwaka na eneo la kwanza ni utalii wa uwindaji kwa kutumia ndege zao wenyewe," alisema Mwambe.

Rais wa Jumuiya hiyo, Dk. Hossam Darwish, alisema jumuiya hiyo imekusudia kuanza uwekezaji kuanzia mwaka huu na tayari wameshakamilisha utafiti katika sekta ya biashara na uwekezaji.

Alisema kuwa wanahitaji kuanza na ujenzi wa Chuo Kikuu cha Masuala ya TEHAMA mkoani hapa ambacho kitakuwa na vitivo 14 ikiwamo biashara, kilimo, teknolojia na digitali.

Alisema jumuiya hiyo itajikita katika uwekezaji wa masuala ya utalii wa uwindaji wanyama na ujenzi wa hoteli zenye hadhi kubwa.

Dk. Darwish alisema katika sekta ya afya watajikita katika ujenzi wa viwanda vya kuzalisha dawa na vifaa tiba, ujenzi wa hospitali za macho na teknolojia ya huduma ya hospitali inayotembea.

Alisema pia wana mpango wa kuandaa maonyesho makubwa maalum ya biashara na uwekezaji nchini ili kuchochea uwekezaji wenye tija.

Aidha, alisema jumuiya hiyo inayo teknolojia ya kisasa ya usindikaji taka ambayo watawekeza kuileta nchini.

# Plan International yawezesha wanawake kuleta mabadiliko

**Na Gwamaka Alipipi**

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Plan International Tanzania katika kipindi cha miaka minne limewawezesha wanawake zaidi ya 100 nchini kuwajengea uwezo wa kujiamini, kuchukua hatua pamoja na kuleta mabadiliko ya kijamii na kisiasa.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Mkuu wa kitengo cha kuwawezesha vijana kiuchumi kutoka Plan International Tanzania, Neema Kiswaga, alisema idadi hiyo ya wasichana imetokana na programu iitwayo 'Girls take over' iliyoanzishwa mwaka 2018.

Alisema kupitia programu hiyo wasichana hupewa fursa ya kujitolea kushika nafasi za uongozi na maamuzi katika taasisi mbalimbali ambazo ni nadra kwa wasichana au wanawake kuzifikia.

Kiswaga alisema kwa mwaka huu wamewafikia wasichana 20 ambao waliweza kushika nafasi za uongozi kwenye taasisi mbalimbali zikiwamo balozi, kampuni za kibiashara, mashirika yasiyo ya kiserikali, mashirika ya umoja wa mataifa pamoja na serikalini.

"Kupitia programu hii tunajenga msichana uwezo kuwa kuchukua maamuzi, kujiamini, kukabiliana na changamoto. Pia kumwondolea vikwazo vya ubaguzi vinavyowarudisha nyuma," alisema Kiswaha.

Alisema kupitia programu hiyo Plan International Tanzania imeweza kuangazia zaidi juu ya suala la unyanyasaji kwa jinsia mitandao ambao kwa sasa imekuwa aina mpya ya unyanyasaji inayoathiri wasichana wadogo.

Kiswaga alisema: "Hii programu imetokana na kampeni ya Girls Get Equal ambayo inalenga kupaza sauti za watoto wa kike na kuhamasisha kwa vitendo hitaji la usawa kwa wasichana kama nyenzo kuu ya kupambana na vikwazo na changamoto kadha wa kadha wanazokumbana nazo katika hatua mbalimbali za maisha zinazotokana na uwapo wa mila, desturi na tamaduni."

Mmoja wa wasichana walionufaika na programu hiyo, Leila Hiza, ambaye ni mhitimu wa kidato cha sita alisema kwa muda wa wiki moja aliyokuwa Kaimu Mkurugenzi amejifunza vitu vingi na kumwondolea woga.


Alisema ameweza kufahamu haki za mtoto wa kike, nafasi ya uongozi pamoja na kuwataka watoto wa kike kutumia vizuri mitandao ya kijamii.

Naye Dorikas John, mnufaika wa programu hiyo, alifanya kazi katika Ubalozi wa Umoja wa Ulaya (EU) kama balozi, alisema: "Katika kipindi chote nilichokuwa pale ubalozini nimejifunza namna ya kuchukua maamuzi. Nimejifunza masuala ya uongozi pamoja na mawasiliano."




Ukurasa 12

Safari robo karne ya mashirika umma kung’ara kileleni nchini, hadi kufifia




Ukurasa 13

Machinga hawajali matiti bali maziwa



Ukurasa 14

Nyerere alivyoshtukia kasi ya kuzaliana nchini akitaka kuwashwa ‘taa nyekundu’

BUFE
IJUMAA OKTOBA 15, 2021
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

# Wanafunzi wahitimu sekondari na zawadi ya ziada elimu ujasiriamali

• Mwekezaji ahamasika kufanya nao kazi

**Na Yasmine Protace,**

MKURANGA

STADI za maisha ambazo zinatolewa shule au vyuoni huwa zinamsaidia mtu kujiongezea kipato kutokana na kupata ujuzi wa aina fulani.

Ujuzi huo ambao mtu anapata, unamwezesha kujiajiri na kujiingizia kipato.

Kutokana na vijana wengi kuhitimu masomo yao baadhi yao wamekuwa wakishinda mitihani, huku wakisumbuliwa na matokeo ya mitihani yao.

Wapo wazazi wanaotumia nafasi hiyo ya watoto wanapomaliza shule au vyuo kuwapeleka tena kujifunza stadi za maisha.

Kuna baadhi ya watoto ambao hawana uwezo wa kufanya kazi zozote hasa wamalizapo shule na vyuo, hali inayosababisha wazazi kuingia gharama za kuwatafutia vyuo kujifunza stadi hizo muhimu kwa maisha ya sasa.

Hivi karibuni katika mahafali ya kidato cha nne ya Shule ya Victory, iliyopo Wilaya ya Mkuranga, mkoani Pwani, Mkurugenzi Mtendaji wa shule hiyo, Peter Mutembe, anasema wameamua kutoa elimu ya stadi za maisha kwa wanafunzi wa shule zote wanazomiliki .

“Wanafunzi wa shule zetu zote tunawafundisha ujasiriamali wa kutengeneza sabuni, mafuta, kupika vyakula vya aina mbalimbali, kutengeneza batiki, kilimo cha mbogamboga, lengo ni kuwezesha mtoto jinsi kujitafutia kipato,” anasema.



Baadhi ya wahitimu wakionyesha batiki wanazotengeneza shuleni Victory, Mkuranga. **PICHA: YASMINE PROTACE**

Anaongeza kuwa wanafunzi hao wanapohitimu masomo, wanaweza kujiajiri na kujikomboa kwa kipato.

Mutembei anafafanua kuwa, mtoto ambaye anakuwa amepata elimu ya ujasiriamali, hata anapomaliza shule hawezi kukaa vijiweni, badala yake atajikita katika kujiongezea kipato.

Mkurugenzi huyo anasema, wahitimu wanapomaliza masomo yao nao hukaa kwa kipindi kirefu wakisubiria matokeo waingie tena katika madarasa mengine.

Anasema katika kipindi ambacho mwanafunzi anasubiri matokeo yake, ndipo anapotumia elimu yake ya stadi za maisha kujiongezea kipato.

**MHITIMU AFUNGUKA**

Fatma Ramadhani, ni mwanafunzi wa kidato cha nne katika shule hiyo, anayeushukuru uongozi wa shule kwa kuandaa masomo ya stadi za maisha.

=Anasema amefanikiwa kujifunza vitu mbalimbali ambavyo alikuwa hajui jinsi ya utengenezaji wake, akiwa na ufafanuzi: “Nilikuwa sijui kupika biriani, kutengeneza mafuta ya kujipaka, kutengeneza dawa ya choo na batiki. Sasa naweza kutengeneza vitu hivyo.”

Fatma anaongeza kwamba, kutokana na kupatiwa elimu ya stadi za maisha, atapomaliza kidato cha nne, ana matarajio ya kujiingizia kipato.

Anasema wapo watoto ambao hawana uwezo wa kupika vyakula na hali hiyo inasababisha kuwarudisha tena darasani, kusoma tena katika vyuo ambavyo vinatoa stadi za maisha.

Anasema elimu ya stadi za maisha itamsaidia kutokana vijiweni na badala yake huo muda watautumia kujiongezea kipato.

**MGENI RASMI**

Mgeni rasmi katika mahafali hayo, Ibrahimu Masome, ambayo ni ofisa masoko kutoka taasisi kubwa ya kibiashara nchini, anakiri kuvutiwa na bidhaa alizozionа kuzalishwa na wanafunzi wa shule hiyo.

Anaahidi asasi yake itaandaa utaratibu wa kuchukua sabuni zinazozalishwa na shule hiyo, ubora ukiangaliwa na kama zitakidhi viwango wataingia ubia wa biashara na shule hiyo.

Pia anawataka wahitimu waendelee na nidhamu wanayofundishwa shule, ili wakichiwa hata mfumo wa kampuni, waweze kuzisimamia kwa weledi.

**MKUU WA SHULE**

Mkuu wa Shule hiyo, Phonsiano Mlelwa, anasema shule imejikita katika kauli mbiu tatu anazozitaja zinasimamia elimu na imegawanyika katika makundi: Elimu ya darasani, elimu ya kujitegemea, usalama na malezi.

“Kuwa na kaulimbiu hiyo inawasaidia wanafunzi kuweza kujiajiri wakimaliza masomo yao na kuacha kuwa tegemezi wakimaliza shule, wanajiajiri wao wenyewe,” anasema.

UNAFAHAMU YA 'SU'?

# Safari robo karne ya mashirika umma kung'ara kileleni nchini, hadi kufifia

**Na Peter Orwa**

MIONGONI mwa yanayokumbukwa katika uongozi zama za Tanzania ya mfumo wa uchumi hodhi na siasa ya chama kimoja, iliyodumu wastani wa miaka 20 ni ustawi wa mashirika ya umma au maarufu 'SU'.

Chimbuko lake kung'ara huko ni uamuzi uliofikiwa mwaka 1964 ulioelekeza nguvu ya serikali pia katika Mpango wa Kwanza wa Maendeleo, ujikite katika kumiliki uchumi.

Maana yake ilijumuisha mamlaka za uzalishaji mali na biashara. Ni wakati ambao Mpango wa Maendeleo wa Kwanza wa Uchumi wa 1964 - 1969, ulinuia nchi kujikomboa kutoka kuegemea uchumi wa kikoloni, yaani "kuzalisha (hasa malighafi ) tusichokitumia na kutumia tusichokizalisha."

Hivyo, suala la kuwa na 'kutumia tunachokizalisha' ina maana ya nchi kuwa na viwanda na mifumo yake yenyewe ya biashara.

Mara moja kwa kutumia mitaji ya ndani, serikali chini ya Rais Julius Nyerere, ilianza kazi huku miaka miwili baadaye sekta ya fedha kupitia kuanzishwa Benki Kuu ya Tanzania (BOT) ilianza kazi na kupata msimamizi wa uhakika, kutoka mikononi mwa Benki Kuu ya Afrika Mashariki.

Pia ni zama iliyoanzishwa Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC), likiwa na jukumu la kusaidia na kulea mashirika. Kabla ya Muungano, ilikuwapo Tanganyika Development Corporation (TDC), ilianzia Januari mwaka 1962.

Uamuzi wa chama tawala TANU mwaka 1967 ulipitisha Azimio la Arusha ambalo lilifilisi rasilimali binafsi kuwa za umma. Hapo kunashuhudiwa ghafla serikali kuanza kuwa na taasisi nyingi za umma.

Mathalan, baada ya Azimio la Arusha, miaka kadhaa baadaye lilizaliwa shirika la kusimamia mali hizo za serikali ambalo liliitwa Msajili wa Majumba, huku benki zilizofilisiwa zilisaidia kuzaliwa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC).

Upande wa pili, juhudi binafsi za Rais Nyerere kupitia nchi marafiki na hasa za Mashariki ikiwamo China, ilipata miradi mingi ya kiuchumi, mfano hai China ilivyosaidia katika ujenzi wa viwanda vya nguo kama Urafiki ya jijini Dar es Salaam.

Pia kuna viwanda vingine vya nguo vilivyowezesha kupatikana mavazi ikiwamo Mutex ya Musoma, Tabotex ya Tabora na Mwatex ya Mwanza, iliyopata kuvuma sana kitaifa.

Kwa kiasi kikubwa mfumo wa



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akikagua ushonaji alipotembelea kiwanda kilichoko jijini Dar es Salaam. Kushoto ni Meneja Mkuu Msaidizi wa kiwanda hicho, Rigobert Massawe. **PICHA: MTANDAO**

> **"Chini ya BIT kuliundwa mashirika kadhaa ya kisekta ikiwamo ya uuzaji vifaa vya majumbani (HOSCO), vifaa vya ujenzi na umeme (BHESCO) na mashirika ya biashara ya mikoa (RTC).**

viwanda hivyo, ni zile kitaalamu iliyoitwa 'Labour Intensive' inayotumia nguvu kazi zaidi kuliko mashine hata kuwezesha kuwa na waajiriwa wengi zaidi, kuliko mbadala wake unaoitwa 'Capital intensive' ambao una hitaji la mashie ziadi kuliko nguvukazi, ambao ndio mfuko unaotumika kwingi zaidi duniani.

Hadi kufika mwaka 1969, hatua kubwa ilishafikiwa katika mageuzi ya viwanda na mashirika ya umma kuongezeka kwa kasi, hapo serikali ikapitisha Sheria ya Kusimamia Mashirika ya Umma (SCOPO), ambayo kwanza ilitoa tafsiri yake.

Kwa mujibu wa sheria hiyo, ni kwamba mashirika yote ambayo serikali ina hisa kuanzia asilimia 51 au zaidi. Pia ni sheria iliyotoa mwongozo wa namna nyingi, ikiwamo katika viwango vya malipo kwa watumishi wa umma.

Hadi kufika mwaka 1971 ambao Rais Nyerere, alitoa hutoba ya kijivunia mno mageuzi ya maendeleo ya mashirika ya umma nchini, kitaifa kuliwapo umma wa waajiriwa waliotapakaa, kinara mkuu akiwa viwanda vya nguo kitaifa.

## MIAKA 10 YA UHURU

Baada ya kufikia miaka 10 ya uhuru nchini, 1971 kulishuhudiwa mageuzi mengine wakati huo, Tanzania ilikuwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Pili (1969 - 1974).

Wakati awamu ya 1964- 1969, ilikuwa ya kuunda mifumo ya uchumi kitaifa inayojitegemea kutoka "tunazalisha tusichokitumia na kutumia tusichokizalisha," awamu ya pili iliangukia katika kuimarisha huduma.

Penye awamu ya pili, mwaka 1973 ndio ikaanzishwa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO). Sekta ya viwanda ilishuhudiwa mambo kadhaa ikiwamo kuundwa mifumo inayowezesha viwanda na mashirika kufanya kazi kwa kujitegemea.

Pia, kuliundwa mashirika ya umma yanayoshikilia nyendo za kiuchumi na uzalishaji, ikishikamana na dira ya mipango kitaifa.

Mapema mwaka 1970 kikao cha Chama cha TANU kilipitisha ajenda ya kuuuga mkono kundi kubwa la wafanyakazi, ikaibuliwa dai la haki yao kwamba kuundwe mabaraza ya wafanyakazi iliyodumu na hata sasa ni sheria inayosimamiwa katika sehemu za kazi.

Ukumbukwe ni katika kipindi ambacho kati ya mwaka 1967 uliofanyika Azimio la Arusha mwaka 1967 hadi 1975, ukiwa unakabiliwa mpango wa pili wa maendeleo nchini, biashara na viwanda zilikuwa chini ya kivuli cha wizara moja.

Mbali na utitiri wa viwanda, pia zilikuwapo kampuni tanzu nyingi zilizoundwa kusimamia maendeo maalum ya uzalishaaji na biashara, ambayo ilisimamiwa kwanza na Shirika la Biashara la Taifa (STC), badaaye ikaundwa Bodi ya Biashara ya Ndani (BIT) na Bodi ya Biashara ya Nje (BET).

Chini ya BIT kuliundwa mashirika kadhaa ya kisekta ikiwamo ya uuzaji vifaa vya majumbani (HOSCO), vifaa vya ujenzi na umeme (BHESCO) na mashirika ya biashara ya mikoa (RTC).

Orodha ya mashirika umma yaliyochipuka, baadhi yake ni yaliyopita kivuli cha NDC kama vile: Shirika la Utalii (TTC), kilichokuwa Kiwanda cha Nyama (TPL), msimamizi wa viwanda vya nguo (NTC), Shirika la Kilimo na Chakula ((NAFCO); Shirika Mipango Ujenzi (NEDCO).

Pia, kuliundwa Bodi ya Korosho (CAT), Shirika la Ujenzi (MECCO), Shirika la Madini (STAMICO) na inayohusika na mbao (TWICO), uzalishaji tumbaku (TTPC), makaratasi (TSN) vifaa vya elimu (TES), mkonge (TSC) na maziwa (TDL), bila kusahau Shirika la Usagishaji la Taifa (NMC) na Shirika la Ugawaji la Taifa .

Ni bahati mbaya kati ya miaka 1974 na 1976 nchi iliapatwa na msukosuko wa njaa hata kuyumbisha mipango na mikakati mingi ya kiuchumi nchini, hata Rais Nyerere alilazimika kwenda kuomba msaada wa chakula nje ya nchi na kupata mahindi ya njano, ambayo yalibatizwa jina 'Mahindi ya Yanga.'

Kuanzia 1976, kulianzishwa Mpango wa Muda Mrefu wa Maendeleo ya Viwanda, ikijumuisha mikakati ya kuwa na aina zote za viwanda; vidogo, vya kati na viwanda mama ambavyo vinazalisha nyenzo za uzalishaji kama majembe.

Ndio pakashuhudiwa kuanzishwa viwanda vya majembe kama UFI cha Ubungo, Dar es Salaam na kingine kama hicho, Mbeya, huku Kibaha kukiwapo kiwanda cha kuunganisha magari.

## TAASISI ZA FEDHA

Mapema kuanzia miaka ya 1970, kulishuhudiwa kuboreshwa taasisi za fedha katika miaka tofauti, ikianziwa na Benki ya Nyumba Tanzania (THB), iliyotanguliwa na NBC ya mwaka 1967, ikifutiwea na nyinginezo kama Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijini (CRDB) na Benki ya Rasilimali Tanzania (TIB), pia kukiwapo Shirika la Bima la Taifa (NIC), nalo lilikuwa kigogo kitaifa katika sekta ya fedha.

Mwaka huu, TIB ambayo pekee ilipona, imeunganishwa na Benki ya Posta (TPB), ambayo nayo kabla zama hizo ilikuwa kitengo cha fedha cha Shirika la Huduma za Posta.

## MAGEUZI YA 1985

Mwaka 1985, awamu ya pili kiserikali nchini iliendana na uchumi wa nchi kuingia katika mfumo huria ulioachwa mwaka 1964.

Ni ndani ya muda mfupi, mfumo wa uchumi ndani ya nchi ikaanza kukabiliana na ushindani mkali wa bidhaa za kigeni, ikianza na nguo za mitumba ambazo zilipitisha kwa kasi utitiri wa viwanda vya nguo vilivyopo.

Kulifanyika mabadiliko makubwa ya kisheria na kuanzia mwisho wa miaka ya 1980 kuruhusu uchumi soko, sambamba na kuporomoka viwanda vingi kitaifa, mfano hai ikiwa jijini Dar es Salaam, foleni kubwa ya wafanyakazi watokao kazini jioni eneo la viwanda, iliyoitwa Barabara ya Pugu, sasa Nyerere wakipungua kila wakati.

Mwanzo wa miaka ya 1990, kulifanyika mabidiliko makubwa ya kisheria yaliyoporomosha kwa kasi mashirika ya umma. Baadhi yake ni katika Sheria ya Fedha na Sheria ya Benki, iliyofanyika katika awamu ya pili ya uongozi wa Rais Ali Hassan Mwinyi, ambayo ilifungulia milango benki binafsi na maduka ya fedha za kigeni.

Wakati huo kulikuwapo maboresho ya kisheria ya BoT, iliyoruhusu kuendana na hali ya uchumi ulioko ndani ya mageuzi ya 1985 nchini.

## KUUNDWA PSRC

Hiyo ilikuwa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma, ambayo iliopewa jukumu la kusimamia mageuzi katika mashirika ya umma, ambayo yashafanyiwa mapitio kisheria mwaka 1992, dhidi ya ile ya mwaka 1969.

PSRC ilipewa majukumu katika sura kuu tatu; yale mashirika ambayo yana hali mbaya ilielekezwa hisa zake zote kuuzwa; pia zile ambazo zinasuasua zilitakiwa kubinafsishwa nusu (51%) auziwe mwekezaji na zilizobaki ni hisa za serikali, pia wananchi waizuwe.

Kwa asasi ambazo ni nyeti sana, zikibinafsiswa kwa mkataba wa muda maalum na kisha baada ya muda imeboreka, serikali ichukue hisa zake.

Ni aina ya ubinafsishaji uliofanywa kwa Shirika la Reli Tanzania (TRC), lakini mwekezaji alishindwa kufanikkisha na akavunjwa mkataba wa miaka 20 aliyopewa, ikarejeshwa serikalini.


Pia, kuna aina ya ubinafshaji ambao hisa zote zilnauzwa kwa wafanyakazi wa taasisi wanaendesha wenyewe, kama ilivyo katika Kiwanda cha Uchapishaji wa Taifa (KIUTA), uwekezaji wao ukilipwa maslahi ya pensheni zao.

Ni bahati mbaya, sehemu kubwa ya wawekezaji wameshindwa kutimiza ama ya mkataba ambayo ni kuboresha uzalishaji, baadhi ya kampuni na viwanda kufa, huku zingine kubadili matumizi, hali inayojidhihirisha leo katika barabara ya Nyerere, mtaa wa viwanda wa zama hizo, leo hii sehemu kubwa imekuwa ni vijiwe vya biashara, vituo vya mafuta na maghala ndio yametawala, hali inayohitimisha umaarufu wa 'SU' kutoweka.



TAFAKURI YA MLALAHOI

# Machinga hawajali matiti bali maziwa






NA JOSEPH KULANGWA
+255 713 410008
jkulangwa@yahoo.com

MTOTO anyonyaye anapohisi njaa, hachagui ni ziwa lipi na la nani la kunyonya, ili mradi ahakikishe njaa inamwondoka.

Hivyo basi, hatajali hata kama ananyonya matiti ya mbuzi au ng'ombe. Anaweza katika umri huo akawa hatambui kuwa aliye naye ni mama yake au siye, ili mradi maziwa yamepatikana.

Nilipata kushuhudia pia mwanakondoo akinyonya matiti ya mama mbwa na hata pale mama mbwa alipokataa, mwanakondoo alimlazimisha kwa kumpiga vichwa mpaka akatulia na akaendelea kunyonya.

Unyonyaji huo huendelea tu hasa pale maziwa yanayonyonywa yanapokuwa haya na madhara yoyote. Na hilo likizoeleka, si ajabu mwana wa binadamu akasusa kumnyonya mama yake akaendelea kumnyonya mama mbuzi au hata mama mbwa, ili mradi kazoea.

Tumeshuhudia kinamama ambao hawataki kunyonyesha watoto kwa muda mrefu, hivyo huwaachisha vichanga wao na kuwazoeza kunyonya chupa. Hakika watoto huzoea na chupa kuwa mama zao na kususa kabisa kunyonya matiti ya mama zao hao.

Mifano hii inaakisi hali ilivyo kwa wafanyabiashara ndogo ndogo waliobatizwa jina la machinga ambao walianzia Dar es Salaam, lakini polepole wakasambaa nchi nzima. Hakuna mkoa usio na machinga kwa sasa.

Wafanyabiashara hawa ni zao la ukosefu wa ajira rasmi, hivyo kuamua kujiajiri na kuita ajira isiyo rasmi. Ni ajira isiyohitaji elimu kubwa, bali ya kujua kuhesabu kinachoingia na kinachotoka.

Ndivyo ilivyoanza, ingawa hivi sasa si ajabu kukutana na machinga mwenye stashahada au shahada mtaani. Yote hayo ni matokeo ya ukosefu wa ajira rasmi. Soma hadi chuo kikuu kisha rudi nyumbani fikiria cha kufanya. Ndio mtindo wa kisasa.

Machinga kwa asili ya biashara yao, hawahitaji kujua wananyonya matiti ya mama yupi. Wanachojali wao maziwa ya natoka au hayatoki? Hata siku moja hawatataka waambiwe eti ghorofani hapa ndipo mahali pazuri pa biashara, wanachotaka wao mteja yupo?

Yawezekana serikali yetu ikawa inafikiria kwa huruma sana, kwamba machinga wanahitaji kufanya biashara yao kwenye maeneo ya kifahari sana. Na hiyo ndiyo ikafanya ije na wazo la majengo makubwa kwa ajili yao.

Tulishuhudia utawala wa Awamu ya Nne ukija na majengo ya Machinga Complex pale Ilala, Dar es Salaam, tena ukiwa na mipango ya kuja na majengo kama hayo Kinondoni na Tabata, ukiamini machinga watakimbilia huko.

Ikakopa mabilioni kujenga mijengo hiyo, lakini hatimaye nini kilitokea? Machinga wakaonja na kutema. Wakarudi mitaani walikozoea kunyonya maziwa ya mama mbwa, ili mradi wanashiba.

Kabla maummivu ya Machinga Complex hayajapoa, utawala wa Awamu ya Tano nao ukaja na lingine la kujenga masoko makubwa makubwa ya mighorofa. Yakajengwa Dodoma, tukasikia Soko la Job Ndugai.

Yakajengwa Morogoro la Chifu Kingalu, la Kisutu, la Magomeni, likaja la Chuno, Mtwara Mikindani, tukasikia la Mwanjelwa, na mengineyo. Mazuri kutazama, mazuri kwa kupamba miji, lakini ni matiti ya mama yasiyotoa maziwa kwa machinga.

Machinga wao wanalilia wateja, hawataki majengo. Juzi kati tukasikia Chifu Hangaya akielezea kuchoshwa na habari anazosikia za masoko kutelekezwa. Akasema basi yageuzwe kumbi za harusi pengine yataingiza kitu.

Ngoja niseme tu hapa, kuna mwaka nilibahatika kwenda kwa wenzetu huko majuu, panaitwa Paris, Ufaransa. Wenyeji wakatuambia mkitaka vitu nafuu tokeni nje ya Jiji, kuna masoko huko pembeni ndiko kuna 'machinga'.

Kweli mimi na wenzangu Wabongo tuliokuwa kwenye msafara huo, tukapanda treni la chini ya ardhi, kama mwendo wa nusu saa hivi tukaibukia juu na kujikuta katikati ya soko la machinga wa Kifaransa, halina maghorofa, bali vibanda kama mahema hivi, tukafanya yetu tukarejea jijini.

Hebu serikali ifanye hivyo basi, hayo maeneo yatengwe nje ya miji, yawekewe mazingira rafiki, huku katikati ya miji yabaki maduka tu yenye bei zao, tuone kama hatutakimbilia kwa machinga kokote waliko! Hebu hili lisingoje keshojama. Maghorofa hayo yageuzwe kumbi za harusi! Alamsiki!

# Nyerere alivyoshtukia kasi ya kuzaliana nchini akitaka kuwashwa 'taa nyekundu'

• Wenye nchi wakaguna, akaahirisha • Dk. Slaa: Ilikuwa moto CCM, nikaitwa

**Na Sanula Athanas**

TANZANIA iko kwenye orodha ya nchi tisa zinazochangia kasi ya ongezeko la watu duniani, ikishika nafasi ya nne barani Afrika.

Wakati hiyo ni taarifa ya mwaka juzi ya Shirika la Umoja wa Mataifa Linaloshughulikia Idadi ya Watu (UNFPA), aliyekuwa Rais wa Tanzania miaka 37 iliyopita, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, alishaiwekea angalizo kwamba mwelekeo wa nchi katika eneo hilo hauko vizuri.

Mwalimu Nyerere alitumia kofia yake ya uenyekiti wa chama katika wakati huo kimeshika hatamu za uongozi, akiibua ajenda aliyotaka iwe msimamo wa chama, kila familia iwe na watoto wasiozidi wanne, hata hivyo suala hilo likazua mtafaruku.

Kimsingi, wakati ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) palikuwa shwari, nje kwenye mifumo ya kijamii, ikiwamo madhehebu, pingamizi nzito ziliibuka.

Ni suala lililofikishwa kama ajenda rasmi kwenye kikao cha Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM (NEC) mwaka 1984, ikiwataka wanaopinga ajenda hiyo ya kitaifa kufafanua pingamizi zao kwa mamlaka muhimu inayofanya uamuzi wa chama, kabla haijawa ajenda ya kiserikali kutekelezwa.

Mamlaka ya CCM wakati huo chama kimeshika hatamu, ilituma ndege maalum kumfuata aliyekuwa Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Dk. Wilbrod Slaa, mkoani Mara alikokuwa kikazi, akaifafanulie NEC mjini Dodoma maudhui ya msimamo wao.

Kwa mujibu wa ufafanuzi wa Dk. Slaa katika kitabu alichoandika mwaka 2019 chenye maudhui ya maisha yake, alifanikiwa kutoa ufafanuzi uliokubaliwa na kikao hicho cha NEC, huku akidokeza msimamo kama wao walikuwa nao Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA).

Hata hivyo, Dk. Slaa anakiri si suala lililopita kirahisi, kwani kupitia wadhifa wake wa Katibu Mkuu wa TEC, kuna wakati alijikuta akiangukia mjadala wa kina na Rais Nyerere ambao wakati mwingine ulichukua kati ya saa sita na saba usiku pasipo mwafaka, akidokeza kuwa ni usiku wa manani.

"Ninaamini sikushughulikiwa kwa kupinga sera hiyo (Sera ya Watu) kwa kuwa hata viongozi wa BAKWATA waliipinga.

"Hata hivyo, msimamo huo ulifanya Mwalimu Nyerere atume ndege maalum kunifuata Musoma kwenda Dodoma kujieleza mbele ya Halmashauri Kuu ya CCM kwanini TEC ilipinga sera hiyo ya kila familia kutozidi watoto wanne," Dk. Slaa anasema katika kitabu chake hicho.



Huduma za kliniki ya watoto zikiendelea, katika moja ya hospitali. **PICHA: MTANDAO**

> **UNFPA kupitia ripoti yake, inatahadharisha haja ya kufanyika udhibiti dhidi ya mwenendo wa kasi kubwa ya watu kuzaana, kundi ambalo Tanzania imo kati ya nchi tisa tajwa.**

### MTAZAMO WA MKAPA

Rais mstaafu wa awamu ya tatu, Hayati Benjamin Mkapa hayuko mbali na wataalamu wanaolia na kasi ya ongezeko la watu dunia, akisema ongezeko la watu ni tishio kwa maendeleo.

Katika kitabu chake cha 'My Life, My Purpose' (Kusudio la Maisha Yangu), Hayati Mkapa anagusia hoja hiyo akieleza shaka yake kuhusiana na kasi ya ongezeko la watu nchini, akishauri kuwe na sera madhubuti ili kuikabili.

Anasema anasikitika kuona suala hilo ni tatizo kubwa si tu Tanzania, bali Bara la Afrika kwa ujumla, huku kukikosekana mjadala wa kutafuta ufumbuzi wake.

Mkapa aliyeiongoza Tanzania kwa miaka 10 kuanzia mwaka 1995, anasema katika kitabu hicho kuwa haoni sera na mwongozo sahihi wa kuikabili ishara hiyo mbaya kwa maendeleo ya umma.

"Ongezeko la watu katika nchi siyo kipimo cha maendeleo bali ni kikwazo kwa maendeleo. Shida kubwa ya nchi nyingi za kiafrika hatuna mjadala madhubuti kuhusu sera ya idadi ya watu katika nchi zetu," Mkapa analalamika.

Kiongozi huyo mstaafu anaeleza ubashiri wa kisayansi wa mwelekeo wa sensa zijazo, kwamba ifakapo mwaka 2025, ambao ndiyo ukomo wa Dira ya Maendeleo ya Taifa, nchi inatarajiwa kuwa na wakazi milioni 67 Tanzania ina eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 947,300.

Juni 1999, Tanzania ilizindua Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ambayo pamoja na mambo mengine, inalenga kupunguza nusu ya watu wanaoishi katika umaskini na kuwafanya wawe katika uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Mkapa anabainisha kuwa wakati wa uhuru mwaka 1961, kulikadiriwa kuwapo Watanganyika milioni 10.4 na idadi iliongezeka hadi milioni 27.4 alipoanza kukalia kiti cha urais mwaka 1995 na iliongezeka hadi milioni 36.1 wakati anaoondoka mwaka 2005.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Tanzania mwaka huu, inakadiriwa kuwa na watu 59,441,988 (milioni 59.44). Kati yao, wanaume ni 29,132,238 na wanawake 30,309,750.

Kwa makadirio hayo, idadi imeongezeka kwa watu milioni 47.1 katika kipindi cha miaka 44 kwa kuwa takwimu za NBS zinaonyesha mwaka 1967, Tanzania ilikuwa na watu milioni 12.3, Tanzania Bara ikiwa na watu milioni 11.9 na Zanzibar watu 354,815.

UNFPA kupitia ripoti yake, inatahadharisha haja ya kufanyika udhibiti dhidi ya mwenendo wa kasi kubwa ya watu kuzaana, kundi ambalo Tanzania imo kati ya nchi tisa tajwa.

Ripoti hiyo inabainisha kuwa Tanzania imo katika nchi tisa zinazochangia kasi ya ongezeko la watu duniani, ikitangazwa kuwa ni ya nne barani Afrika.

UNFPA inaitaja India, taifa linalokadiriwa kuwa na watu bilioni 1.38 mwaka huu, ndiyo ya kwanza kwa kasi kubwa ya ongezeko la watu na katika mataifa nane yanayofuata, matano ni ya barani Afrika na matatu ni ya kusini mwa Jangwa la Sahara na mawili ni wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Orodha ya mataifa hayo kwa nafasi zake nyuma ya India ni Nigeria; Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC); Pakistan; Ethiopia; Tanzania; Marekani; Uganda na Indonesia.

Vilevile, ripoti inasema wakazi wa dunia wataongezeka kutoka bilioni 7.6 wa mwaka 2016 hadi bilioni 8.6 ifikapo mwaka 2030, ambao ni ukomo wa kipindi cha Malengo ya Maendeleo Endelevu.

### WACHUMI

Wataalamu wa mipango ya uchumi wanaweka wazi kwamba, kinachoshuhudiwa sasa nchini kukiwa na uhaba wa ajira na migogoro mingi ya ardhi nchini, ni matokeo ya ongezeko la watu.

Mathalani, Mkuu wa Kitengo cha Hazina cha Benki ya Biashara Kenya (KCB) Tawi la Tanzania, Pascal Machango, ananyooshea kidole uhaba wa ajira nchini kwamba unazalishwa katika uwiano usio sawa kati ya kasi ya kukua kwa uchumi na idadi ya wahitaji wa ajira, kwa maana ukuaji wa uchumi unapaswa kuzalisha fursa za ajira kuutumikia.

Machango anasema kwa sasa kunashuhudiwa ongezeko kubwa la idadi ya watu nchini lisiloendana na fursa za ajira zilizopo.

**SENSA TANZANIA**

| Mwaka | dadi ya watu | Tanzania Bara | Zanzibar |
|---|---|---|---|
| 1967 | 12,313,469 | 11,958,654 | 354,815 |
| 1978 | 17,512,610 | 17,512,610 | 476,111 |
| 1988 | 23,095,878 | 22,455,193 | 640,685 |
| 2002 | 34,569,232 | 33,584,607 | 984,625 |
| 2012 | 44,928,923 | 43,625,354 | 1,303,569 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)





# Samia apongezwa utatuzi wa kero

Na Peter Mkwavila, DODOMA

JUMUIYA ya maridhiano mkoani Dodoma imesema katika kipindi cha miezi sita ya uongozi, Rais Samia Suluhu Hassan amelibadilisha taifa katika masuala ya kimataifa na kufanikisha kushawishi Shirika la Fedha Duniani (IMF) kutoa Sh. Trilioni 1.3 ambazo zitakazochochea kwa kasi maendeleo ya taifa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa, Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Askofu Evance Chande, alisema uamuzi wa Rais Samia kuelekeza fedha hizo kwenye sekta muhimu zinazowagusa wananchi wa kipato cha chini ni jambo la kupongezwa.

Chande aliwataka wasimamizi wa miradi upande wa serikali kuepuka mazingira ya rushwa na wizi.

"Tumemsikiliza vizuri kwenye hotua yake ilisheheni majibu mazuri ya maswali ya Watanzania, hivyo hatuwezi kunyamaza kana kwamba hatujasikia chochote bila kutoa pongezi nyingi kwa Rais wetu tunakupongeza sana, ulikuwa umenyamaza kumbe ulikuwa unaweka mambo sawa, hongera sana Rais wetu.

"Fedha hizo zimeelekezwa kwenda kujenga shule za msingi, madarasa ya sekondari, vifaa tiba na mitambo ya hospitali hatua ambayo inakwenda kuimarisha sekta ya afya hasa kipindi hiki cha janga la corona ambapo kulikuwa na upungufu wa mitungi ya gesi ya oksijeni na dawa," alisema.

Katika sekta ya maji, alisema Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), imefanya kazi kubwa, lakini Rais ametenga fedha kwa ajili ya kununua mitambo ya kuchimba visima vijijini.

"Tunafahamu tatizo la maji vijijini ni kubwa na gharama za kuchimba visima ni kubwa, ninaamini kuwa ununuzi wa mitambo ya kuchimba visima itaenda sambamba na upatikanaji wa maji kwa ajili ya kilimo cha mboga mboga vijijini, sote tunatambua kuwa maji safi yakipatikana yanaleta tija kwa wanakijiji na kupunguza magonjwa ya milipuko kama kipindupindu," alisema.

Askofu Chande alisema pamoja na kwamba Rais Samia amesema viatu vya Hayati Magufuli ni vikubwa, wanaona anatembea kwenye nyayo zake.

Alimpongeza Rais kwa kuelekeza miradi yote itakayotekelezwa kupitia fedha hizo itekelezwe na wazawa kwa kutumia mafunzi wa mitaani hivyo itasaidia kuongeza ajira kwa mafundi na vibarua wake.

# Halmashauri zabanwa utekelezaji miradi ya ufadhili fedha za IMF

Na Paul Mabeja, DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imeagiza mikoa na halmashauri kutoa taarifa ya utekelezaji wa miradi kupitia fedha zilizotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF) kila baada ya wiki mbili.

Sambamba na kutoa taarifa, ofisi hiyo imetoa maagizo 12 kuhusu utekelezaji wa miradi hiyo na kutaka itekelezwe kwa wakati.

Shirika hilo limeipatia Tanzania Sh. trilioni 1.3 kwa ajili ya kampeni ya maendeleo kwa ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya corona ili kuchangia kufufua uchumi kwa sekta zilizopata athari za kiuchumi kutokana na madhara ya ugonjwa huo.

Akizungumza juzi na waandishi wa habari jijini hapa, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, Ummy Mwalimu, alisema kati ya fedha hizo, ofisi yake imeidhinishiwa Sh. bilioni 535.68 kati ya hizo, Sh. bilioni 304 ni kwa ajili ya elimu msingi, Sh. bilioni 226.68 afya ya msingi na Sh. bilioni tano ni kwa ajili ya kuboresha miundombinu na mazingira ya kufanyia biashara kwa wafanyabiashara wadogo.

Maagizo mengine ni pamoja na kuunda Kamati ya Mkoa ya Uratibu na Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi husika na kuhakikisha taarifa za utekelezaji wa miradi hiyo zinawasilishwa kwa Katibu Mkuu TAMISEMI kila baada ya wiki mbili.

Waziri huyo alizitaka halmashauri kuhakikisha miradi ya ujenzi wa madarasa inakamilika kabla au ifikapo Desemba 15, mwaka huu na miradi mingine ikamilike ifikapo Aprili 30, mwakani.

"Halmashauri zinatumia makandarasi wa ndani au utaratibu wa 'force account'. Hata hivyo, ninasisitiza gharama za utekelezaji kwa kutumia njia yoyote zisizidi makadirio ya fedha zilizotengwa kwa shughuli husika," alisema.

Alisema halmashauri zitakazotaka kufanya mabadiliko ya utekelezaji wa eneo la mradi, maombi yawasilishwe kwa maandishi kwa Katibu Mkuu TAMISEMI ndani ya wiki moja baada ya kupokea fedha hizo.

"Utekelezaji wa miradi yote uzingatie thamani ya fedha na ubora wa miradi, watoa huduma wa vifaa, mafundi watangaziwe kazi zilizopo kupitia tovuti za mikoa, halmashauri pamoja na mbao za matangazo katika ofisi za umma," alisema.

Ummy alisema halmashauri zinaelekezwa kufanya ununuzi wa pamoja ili kupunguza gharama za utekelezaji wa miradi.

Kadhalika, aliagiza mameya na wenyeviti wa halmashauri pamoja na madiwani kupitia kamati zao wahakikishe wanasimamia miradi hiyo kwa kushirikiana na watendaji wa halmashauri.

"Wakurugenzi wa halmashauri wahakikishe miradi yote iliyokamilika na ununuzi wa vifaa zinawekwa alama ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi na Mapambano dhidi ya Uviko-19 (corona)," alisema.

Alihimiza wananchi kushiriki ujenzi wa miradi inayoendelea katika maeneo yao na kutoa taarifa endapo kuna ubadhirifu wa fedha.




Mkurugenzi Mtendaji wa kiwanda cha kuzalisha mafuta ya kula cha Pyxus Agriculture Tanzania, Malcom Mcgrath (kulia), akimpa maelezo Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo (kushoto), alipotembelea kiwanda hicho, jijini Dodoma juzi. PICHA: IBRAHIM JOSEPH

# Wadau wataka nguvu elimu ya corona

Na Augusta Njoji, DODOMA

WADAU wa Kongamano la Afya nchini (THS), wameshauriwa kuongeza nguvu ya utoaji elimu kwa jamii ili kupambana na ugonjwa wa corona.

Akizungumza jana baada ya kuwasilisha mada mbalimbali kwenye kongamano hilo, Meneja wa Mradi wa HPSS-Tuimarishe Afya unaotekelezwa na Shirika la Maendeleo la Ushirikiano la Swiss (Swiss TPH), Ally Kebby, alisema hatua hiyo itasaidia kuunga mkono jitihada za serikali katika kukabiliana na ugonjwa huo kwa kutoa chanjo kwa wananchi.

Kebby alisema serikali imeonyesha juhudi za kuwakinga watu wake na kuzuia maambukizi ambapo chanjo 900,000 zimetolewa na kazi inaendelea na imepokea chanjo zingine.

Meneja huyo alisema jukumu la wadau wakiwamo wananchi ni kufanya maamuzi sahihi ya kujikinga, kuchanja na kufuata njia zingine za kujikinga zinazotolewa na wataalamu wa afya.

"Katika utekelezaji wa mradi huu, shirika limeshirikiana na serikali katika kupambana na magonjwa ya mlipuko kama vile kipindupindu mwaka 2015, kuzuia kwa ugonjwa mkali wa ini uliotokana na sumu kuvu mwaka 2016, VVU na janga la corona.

"Tangu kesi ya kwanza ya maambukizi ya corona nchini Tanzania iliripotiwa Machi 2020, HPSS imeshiriki na serikali kupitia mpango wa dharura wa kukabiliana na ugonjwa huu kwa kushiriki kutoa elimu kwa jamii,"alisema.

Awali, akizungumzia mwitikio wa kujiunga na Bima ya Afya ya Jamii (CHF iliyoboreshwa), Elizeus Rwezaura, alisema idadi ya wanachama wa iCHF imeongezeka na kufikia watu 3,032,007 mwisho wa Julai, mwaka huu.

|rwezaura alisema hadi kufikia Juni, mwaka huu, mapato yaliyokusanywa kwenye vituo vya kutolea huduma ya afya yaliongezeka hadi kufikia zaidi ya Sh. bilioni 11.81.

"Bado sera haijaweka wazi upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kuendelea kuimarisha iCHF, jambo ambalo linatoa tahadhari ya kuwa bila kuwepo ruzuku kutoka nje ya mfuko," alisema.

Alisema uimara wa kifedha utategemea tu kiwango cha michango ya uandikishaji na wanachama kufikia asilimia 30 ili kugharamia huduma ipasavyo.





# Magari 200 ya mizigo yakwama mpakani

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

ZAIDI ya malori 200 yanayosafirisha mizigo kati ya Tanzania na Malawi, juzi yalikwama katika mpaka wa Kasumulu wilayani Kyela kutokana na sababu ambazo hazijulikani.

Hali hiyo iliwafanya madereva wa malori hayo kuiomba serikali kuingilia kati.

Nipashe lilifika katika eneo hilo na kukuta malori hayo yamefungiwa ndani ya geti mpaka majira saa 2:00 asubuhi ambapo Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Magereza, Ismail Mlawa, aliingilia kati ya kuamuru yafunguliwe.

Pamoja na amri hiyo ya Mkuu wa Wilaya, bado geti halikufunguliwa haraka kutokana na mmoja wa maofisa wa kituo cha forodha cha mpaka huo kudaiwa kuwa aliondoka na funguo hali iliyowafanya madereva kutaka kufanya fujo.

Baadaye alitokea ofisa mmoja akafungua geti kisha magari yakaruhusiwa kutoka katika eneo hilo huku baadhi ya madereva wakidai kuwa walikwama kwa zaidi ya wiki moja bila sababu za msingi. Mmoja wa madereva hao, Musa Seif, alisema tatizo hilo limedumu kwa zaidi ya mwezi sasa na kwamba kitendo cha maofisa hao kuyarundika magari hayo ndani ya eneo hilo na kuyafungia ni hatari endapo itatokea ajali ya moto.

Alisema tatizo hilo lipo kwa upande wa Tanzania pekee lakini wakivuka upande wa Malawi hakuna tatizo kama hilo bali magari yanakaguliwa na taratibu zingine kisha wanaruhusiwa kuendelea na safari.

Seif alisema kama eneo hilo halitoshi ni vyema likaandaliwa eneo nje ya kituo hicho cha forodha kwa ajili ya maegesho ili katika eneo hilo la yapite magari yaliyokamilisha taratibu na kuruhusiwa kuvuka.

"Haya sasa kama mlivyoona Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya amefika hapa anataka geti lifunguliwe lakini mtu ameondoka na funguo. Likitokea janga la moto hapa uokoaji utafanyikaje na je, kwa mrundikano huu wa malori magari ya zimamoto yatapita wapi?" Alihoji Seif.

Jonard Msangi alisema kitendo cha kukwama katika eneo hilo kwa muda mrefu kinasababisha gharama za maisha kuongezeka kutokana na siku za safari kuongezeka na wao kutakiwa kulala siku nyingi kwenye eneo moja.

Alisema mbali na kukwamishwa na maofisa wa serikali katika eneo hilo, pia kuna baadhi ya huduma ambazo wanapata katika eneo hilo wanalipia ikiwamo choo, hivyo hali kuzidi kuwa ngumu.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alizungumza na waandishi wa habari, alionyeshwa kukerwa na kitendo cha magari hayo kukwama, hivyo kuagiza yaruhusiwe kuondoka.

Homera alisema katika uchunguzi wake alibaini kuwa utendaji wa watumishi wa kituo cha forodha cha Kasumulu unatakiwa kufanyiwa maboresho.

"Nimeshatoa maelekezo ya kuboresha utendaji katika mpaka ule. Moja ya maelekezo yangu ni kuongeza muda wa kufanya kazi kituo kitafunguliwa saa 11:00 alfajiri na kufungwa saa 4:00 usiku ili kupunguza msongamano wa magari. Pia tumewaomba na wenzetu Malawi waongeze muda," alisema Homera.

Alisema pamoja na maagizo hayo, kuna mambo anaendelea na uchunguzi wa baadhi ya mambo ambayo hayako vizuri kwenye eneo hilo na kwamba yanaweza yakasababisha uhusiano na Malawi kuzorota.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (watatu kushoto), akizungumza na Balozi wa Malawi hapa nchini, Glad Munthali (kulia) pamoja na Naibu Waziri wa Ujenzi na Usafirishaji wa Malawi, Nancy Chaoli (katikati), wakati wa ziara ya viongozi hao, mkoani humo juzi, iliyokuwa na lengo la kuimarisha ushirikiano wa kidiplomasia na kibiashara. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Naibu waziri Malawi afanya ziara mkoani Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi wa Malawi, Nancy Chaola, amefanya ziara mkoani Mbeya kwa lengo la kuimarisha ushirikiano wa kidiplomasia kati ya Tanzania na nchi yake.

Ziara hiyo pia ina lengo la kuimarisha ushirikiano wa kibiashara baina ya mataifa hayo mawili.

Katika ziara hiyo iliyofanyika juzi, Chaola aliongozana na Balozi wa Malawi nchini Tanzania, Glad Munthali, na maofisa mbalimbali wa serikali ya Malawi na kupokewa na mwenyeji wao, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera.

Viongozi hao walianza ziara katika Wilaya ya Kyela na walipokewa katika mpaka wa Kasumulu kisha kutembelea Bandari ya Kiwira ambayo ndiyo Makao Makuu ya Bandari za Ziwa Nyasa.

Baada ya kutembelea bandari hiyo, viongozi hao walifanya mazungumzo na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kabla ya kusafiri mpaka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe ambako walitembelea na kukagua miundombinu mbalimbali.

Aidha, Naibu Waziri huyo wa Malawi akiwa ameongozana na mwenyeji wake, Homera. walitembelea Bandari Kavu ya Malawi iliyoko katika eneo la Iyunga jijini Mbeya kwa ajili ya kujionea utendaji kazi kabla ya kurejea Malawi.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuhitimisha ziara hiyo, Naibu Waziri Chaola alipongeza Tanzania kwa uwekezaji ilioufanya kwenye miundombinu huku akisema itawasaidia hata wao kufanya shughuli zao.

"Malawi haiwezi kuendelea bila Tanzania kwa sababu nchi yetu haina bandari. Tunategemea mizigo yetu iingie kupitia Bandari ya Dar es Salaam na kisha kusafirishwa kwa njia ya barabara kwenda nchini kwetu, kwa hiyo tunaiomba serikali ya Tanzania iendelee kutupa ushirikiano," alisema.

Chaola alishauri usafiri wa reli ya TAZARA uimarishwe ili mizigo ya Malawi iwe inasafirishwa kwa njia hiyo mpaka Mbeya na kisha kuvuka mpaka kwa njia ya barabara.

Pia aliiomba serikali ya mkoa wa Mbeya kuimarisha biashara ya ndizi kwa kujenga vituo maalumu vya kuuzia ili kuwarahisishia wafanyabiashara wa Malawi kupata bidhaa hiyo. Alisema kwa sasa Malawi haina ndizi kutokana na ugonjwa wa ajabu kuharibu zao hilo.

Waziri huyo aliiomba serikali ya Tanzania kupitia Shirika la Ndege (ATCL) kuanzisha safari za ndege za kwenda Malawi kwa kuanzia Dar es Salaam- Mbeya-Lilongwe na kwamba uwanja wa Songwe utakuwa kiunganishi kizuri kati ya mataifa hayo.

Homera alimpongeza Waziri Chaola kwa ziara hiyo na kusema itasaidia kuimarisha ujirani mwema na kufungua fursa za kibiashara baina ya mataifa hayo mawili.

Homera alisema ili kuimarisha zaidi ushirikiano huo, wanajiandaa kufanya mkutano wa ujirani mwema hivi karibuni ambao utaratibiwa na serikali zote mbili na utafanyika Tanzania ua Malawi kulingana na makubaliano ya pande zote.

Alimwomba waziri huyo kuwashawishi wafanyabiashara wa Malawi kusafirisha mizigo yao kwa kutumia meli mbili za mizigo zilizojengwa na serikali katika Ziwa Nyasa.

Naye Balozi Munthali alisema wananchi wa Tanzania wanaonyesha upendo mkubwa kwa raia wa Malawi na wanawakirimu vizuri wanapoingia kwa ajili ya shughuli mbalimbali zikiwamo za kibiashara.

# Jiji Mbeya latoa mikopo mil. 569/-

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya imetoa mkopo wenye thamani ya Sh. milioni 569 kwa vikundi 62 vya wajasiriamali wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ambazo ni asilimia 10 ya mapato ya ndani.

Akikabidhi mikopo hiyo juzi, Meya wa Jiji hilo, Dor Mohamed Issa, alisema fedha hizo ni sehemu ya utekelezaji wa sheria ya kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani ambayo yanagawanywa kwa utaratibu wa asilimia nne vikundi kwa wanawake, nne vijana na asilimia mbili vikundi vya walemavu.

Meya Issa alisema lengo la kutoa mikopo hiyo ni kuviinua vikundi hivyo vya wajasiliamali kiuchumi na kwamba halmashauri hiyo imekuwa ikitekeleza utaratibu huo kila robo ya mwaka.

"Tunatoa mikopo hii kwa ajili ya kuvisaidia vikundi hivi kuondokana na umasikini. Serikali ilileta utaratibu huu kwa lengo maalumu na tutaendelea kutekeleza matakwa haya ya kisheria," alisema Issa.

Mbunge wa Mbeya Mjini ambaye ni Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, alivitaka vikundi vilivyonufaika na mkopo huo kuhakikisha vinarejesha kwa wakati ili vikundi vingine vinufaike kama wao.

Alisema kumekuwa na tatizo la baadhi ya vikundi kutorejesha mikopo kwa wakati, hivyo kukwamisha malengo ya serikali ya kuvifikia vikundi vingi zaidi.

"Mikopo ya benki watu mnarejesha kwa wakati na hata kwa wakopeshaji wengine wenye mikopo yenye riba mnarejesha lakini tatizo lipo kwenye hii mikopo ya halmashauri. Wengi hamrejeshi kwa wakati, hivyo tunaomba mjitahidi sana," alisema Dk. Tulia.

Aliwataka wananavikundi hao kuhakikisha wanafanya biashara zao kwa kufuata taratibu ili wapate faida na warejeshe mikopo yao na kuendeleza maisha yao.



# Mwinyi kuendeleza uhusiano na Comoro

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema Zanzibar iko tayari kuendeleza uhusiano na ushirikiano wa kihistoria uliopo kati yake na Muuungano wa visiwa vya Comoro hasa katika sekta za maendeleo ikiwamo ya biashara.

Rais Dk. Mwinyi aliyasema hayo juzi Ikulu Zanzibar, wakati alipokutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Muungano wa visiwa vya Comoro nchini Tanzania, Dk. Ahamada El Badoi Mohamed Fakih. Katika mazungumzo hayo, Rais Dk. Mwinyi alisema kwamba kutokana kuwepo kwa mahusiano ya kidugu baina ya pande mbili hizo ni kichocheo pekee cha wafanyabiashara wa Zanzibar na Comoro kuimarisha sekta ya biashara hasa kutokana na mwingiliano wa kidugu uliopo.

Alisema serikali anayoiongoza pamoja na wananchi wake itaendeleza na kudumisha uhusiano na ushirikiano huo wa kihistoria uliopo sambamba na kuendeleza sekta za uchumi kwa ushirikiano wa pamoja kwa maslahi ya nchi mbili hizo na watu wake.

Naye Balozi wa Comoro nchini Tanzania, Dk. Mohamed, alisema ipo haja ya kurudisha utamaduni wa wafanyabiashara wa nchi hizo mbili kufanya biashara pamoja.

Alisema uhusiano na ushirikiano wa kihistoria uliopo kati ya Comoro na Zanzibar una kila sababu ya kuimarishwa zaidi kwa maslahi ya pande zote mbili.

Alimweleza Dk. Mwinyi azma ya nchi yake ya kutekeleza mkataba wa makubaliano kati ya Zanzibar na Comoro katika uongozi wa awamu iliyopita huku akitoa shukrani kwa huduma kadhaa wanazozipata wananchi wa nchi yake katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zikiwamo huduma za afya, elimu na zingine.

Katika hatua nyingine Rais Mwinyi alikutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Namibia nchini Tanzania, Lebbius Tangeni, aliyefika Ikulu kujitambulisha na katika mazungumzo hayo viongozi hao walisisitiza haja ya kuwapo ushirikiano wa pamoja hasa katika uendelezaji wa sekta za kiuchumi ikiwamo viwanda, biashara, uwekezaji pamoja na uhusiano wa miji na manispaa za Zanzibar na Namibia.

Pia Rais Mwinyi alikutana na kufanya mazungumzo na Mwanasheria Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Jaji Dk. Elieza Mbuki Feliesh ambaye alifika Ikulu kwa ajili ya kujitambulisha.

# JUMAZA yazungumzia pingamizi la serikali

**Na Mwandishi Wetu**

WAKILI wa Jumuiya ya Maimamu Zanzibar (JUMAZA), Omar Shehe Omary, amesema kusudio la kuishtaki serikali imetolewa tangu Febuari 8, mwaka huu kabla ya mashtaka dhidi ya Mwanasheria Mkuu na Bodi ya Udhibiti Vileo baada ya kuvunja Sheria ya Vileo Namba 9 ya Mwaka 2020.

Omary alisema hayo wakati wa kusikiliza pingamizi zilizofunguliwa na upande wa serikali wakidai kesi hiyo imefunguliwa bila ya kutolewa kusudio la siku 60 ya kushtaki serikali kinyume na sheria.

Alisema hoja ya kukosekana tarehe ya siku kiapo kulifanyika katika hati ya maombi ya wateja wake sio kosa la kumfanya mtu kukosa haki yake wakati ni jambo linaloweza kurekebishwa ili kuhakikisha haki inatendeka katika kesi ya msingi. Alisema kesi dhidi ya Mwanasheria Mkuu SMZ na Bodi ya Vileo imefunguliwa na wateja wake kwa kuzingatia kifungu cha 23(1) na 24 (1) vya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 baada ya Bodi ya Vileo kuvunja sheria namba tisa ya mwaka 2020.

Wakili Omar alisema kwa mujibu wa kifungu cha 28 (1) cha sheria namba tisa ya vileo, baa zinatakiwa umbali wa mita 1000 kutoka maeneo ya huduma za jamii kabla ya kupewa leseni ya biashara ikiwemo na kukaa mbali na nyumba za ibada, shule hospitali na makazi.

Alisema kimsingi sheria imetungwa na SMZ akiwamo mwanasheria mkuu na inapaswa kufuatwa na kuiheshimu kama ilivyotungwa na kupitishwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

"Mheshimiwa Jaji hoja ya pingamizi ya kutaka ashtakiwe Mwanasheria Mkuu SMZ kwa jina badala ya taasisi yake haina msingi wa hoja. Naomba pingamizi zote zitupiliwe mbali tuendelee na kesi ya msingi," alisema Wakili Omary. Awali akiwasilisha pingamizi zake Mwanasheria wa Serikali kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Ali Issa Abdalla, alisema kesi hiyo imefunguliwa kinyume na sheria bila ya kutolewa kusudio la siku 60 ya kushtaki serikali.

Alisema barua ya Febuari 8, mwaka huu ya indhari inaonyesha ilitolewa na Jumuiya ya Maimamu Zanzibar (JUMAZA) wakati kesi ya msingi imefunguliwa na Bodi ya Wadhamini ya Jumuiya ya Maimamu Zanzibar.

Aidha, alisema kuwa katika kesi hiyo alipaswa kushtakiwa Mwanasheria Mkuu kwa jina lake badala ya jengo la Mwanasheria Mkuu na watu kwa mujibu wa kifungu cha sita cha sheria namba tatu ya mwaka 2010.



Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud, akipata maelezo kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Muhamed Mahmoud (mwenye suti nyeusi), kuhusu athari za kimazingira za mabadiliko ya tabianchi katika fukwe ya bahari ya Nungwi jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Watendaji watakiwa kudhibiti uharibifu mazingira

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar Othman Masoud Othman, amewaagiza watendaji wa Shehia, wilaya na mikoa kutumia mbinu mbadala za kushughulikia na kudhibiti uharibifu wa mazingira unaotokana na uchimbaji holela wa mchanga katika maeneo mbalimbali ya Zanzibar.

Aliyasema hayo jana kwa nyakati tofauti wakati akiwa katika mfululizo wa ziara yake ya kukagua uharibifu wa mazingira unaotokana na mabadiliko ya tabianchi pamoja na shughuli za kibinadamu.

Alisema kuwapo kwa mbinu mbadala kutasaidia kukabiliana na uharibifu wa mazingira na kupunguza kasi ya tatizo hilo linalojitokeza katika maeneo mbalimbali nchini.

Aliwataka watendaji hao kufahamu rasilimali ya mchanga inayochimbwa maeneo mbalimbali haiuzwi nje na ni dhahiri kwamba inahitajika kwa matumizi ya kijamii, na ni busara viongozi katika maeneo yao kwa kufuata utaratibu kutenga maeneo na kuyarasimisha kwa matumizi ya shughuli za kijamii zinazotumia rasilimali hiyo.

Alisema maeneo mengi nchini yameharibiwa na yana mashimo makubwa yaliyosababishwa na vijana wanaochimba mchanga kinyume na sheria licha ya wahusika wa vitendo hivyo kufahamika.

Alisema ni vyema sehemu zilizoharibika zikatafutiwa mbadala wa kurekebishwa ikiwa ni pamoja na kufanya juhudi kupandwa miti ili kuepusha kubakia kama zilivyoharibiwa na kuleta athari zaidi.

Akitembelea ushirika wa wenye mashamba Jozani, unaojishughulisha na ufugaji wa samaki, kasa na makobe, Makamu amewapongeza kwa kazi kubwa wanayofanya na kuutaka uongozi wa ushirika huo kujitangaza zaidi ili fursa kubwa ya biashara ya utalii iliyopo katika eneo hilo kufahamika na kuwanufaisha zaidi.

Aliutaka uongozi unaosimamia dampo la kisasa, Kibele Wilaya ya Kati Unguja, kulitunza na kuendeleza ili juhudi zilizofanywa ziweze kutimiza dhamira na lengo kuanzishwa kwa dampo hilo kwa kuzingatia hifadhi ya mazingira nchini.

Alitaka hatua za kitaalamu zichukuliwe kuhakikisha dampo hilo linaendelezwa vyema na kutimiza malengo ya kuanzishwa kwake ikiwa ni pamoja kuwapo ubunifu wenye tija sambamba na kuzikabili changamoto zilizopo kwa kuzingatia kuwa limetayarishwa kwa uwekezaji mkubwa wa msaada wa washirika wa maendeleo.

Naye Meneja wa dampo hilo, Hassan Mohammed Ali, alisema licha ya kuwapo mafanikio makubwa ya sehemu rasmi ya kutupia taka inayozingatia hifadhi ya mazingira, lakini limekabiliwa na uhaba wa wafanyakazi na kukosekana kwa bajeti ya kutekeleza masuala mbalimbali ya kiutendaji.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Kati Unguja, Marina Joel Thomas, alisema licha ya kuwapo juhudi kubwa zinazofanywa na serikali ya wilaya kuwadhibiti vijana wanaofanya uharibifu wa mazingira ikiwa ni pamoja na kufanikiwa kuwakamata baadhi ya vijana, bado tatizo hilo linaendelea kujitokeza katika maeneo tofauti wilayani humo.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Kusimamia Mazingira Zanzibar Sheha Mjaja, alisema utafiti unaonyesha kwamba maeneo mbalimbali ya fukwe za Zanzibar ikiwamo Jambiani, Nungwi, Kisiwapanza na Msuka ndiyo yameatharika zaidi na tatizo la mazingira kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

# DC akibana kiwanda kulipa wafanyakazi

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

UONGOZI wa Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma umeutaka uongozi wa kiwanda cha kubangua korosho kinachomilikiwa na kampuni ya Korosho Africa kulipa kiasi cha Sh. milioni 246.574 kwa wafanyakazi wake 600 ambao wamekuwa wakilalamikia kupunjwa stahiki zao.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Julius Mtatiro, alitoa maagizo hayo alipotoa mrejesho wa taarifa ya tume aliyoiunda kwa ajili ya kuchunguza malalamiko hayo baada ya kiwanda hicho kufungwa Septemba mwaka jana.

Alifafanua kuwa kutokana na hesabu zilizopigwa, kila mfanyakazi anatakiwa kulipwa kiasi cha Sh. 400,000 ikiwa ni fedha ya nyongeza kwa wafanyakazi wa kiwanda hicho baada ya kamati kubaini kuwapo kwa kosa la uongozi wa kiwanda kuwakalisha kwa miezi minne bila kupewa notisi ya siku 28 kabla ya kufunga kiwanda chao.

Alisema kwa kufanya hivyo, uongozi wa kiwanda ulikiuka sheria kazi inayoelekeza endapo mfanyakazi ataondolewa bila kufuta taratibu, atatakiwa kulipwa stahiki kulingana na kima cha chini cha mshahara wake. Alisema kiasi hicho cha fedha kinatakiwa kulipwa kwa wafanyakazi wote 600 ifikapo Oktoba 27, mwaka huu, vingine ofisi yake itaufikisha mahakamani uongozi wa kampuni hiyo.

Mbunge wa Tunduru Kaskazini, Hassan Kungu, aliwataka wafanyakazi hao kuwa wavumilivu wakati suala hilo likiwa linatafutiwa ufumbuzi.

Baadhi ya wafanyakazi hao waliishukuru serikali kwa kuwa mwanga wa kupata stahiki zao umeonekana, lakini kuna kundi dogo lingine ambalo linaamini huenda hayo ni maneno tu na hayana ukweli wowote.




Meneja Uhusiano wa Airtel, Jackson Mmbando (kushoto), akizungumza jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kampuni hiyo, kutoa faida ya 2.1bn/- kwa wateja pamoja na Mawakala wa Airtel Money kwa kipindi cha robo mwaka kuanzia Aprili hadi Juni 2021. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakesha kusaka maji kisa bwawa kukauka

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAKAZI wa Kijiji cha Lukenge Kata ya Magindu wilayani Kibaha, wanakesha kutafuta maji kwa miezi minne sasa kutokana na bwawa walilokuwa wakilitegemea kukauka.

Wakizungumza na waandishi wa habari waliofika katika eneo hilo jana, wananchi hao walisema wanashindwa kufanya shughuli za maendeleo pamoja na kuhudumia familia kutokana na muda mwingi kuutumia kusubiri maji kwenye visima walivyochimba katika bwawa hilo.

Eliza Mrisho, mmoja wa wananchi waliokuwa wakisubiri maji katika visima hivyo, alisema ametumia siku tatu kuanzia saa 11 alfajiri hadi saa 12 jioni kusubiri maji ambayo kwa siku zote hizo ameambulia madumu mawili ya lita 20 kutokana na maji yanayopatikana na foleni iliyopo.

"Nyumbani nina mzazi ambaye ametoka kujifungua hata maji ya kumwogeshea na kumpikia uji sipati. Muda wote nashinda kisimani kusubiri maji. Sihudumii familia, mifugo inakufa kila siku kwa kukosa maji. Hali katika kijiji chetu ni mbaya serikali itusaidie katika hili," alisema.

Mkazi mwingine, Tatu Shabani, alisema maji yamekuwa chanzo cha kukwamisha shughuli za wananchi lakini pia wanapata magonjwa ya mlipuko kutokana na maji wanayotumia kutokuwa salama.

"Bwawa hili ni la kwanza kuzinduliwa na Hayati Rais Benjamini Mkapa mwaka 2001 tangu kipindi hicho halijawahi kufanyiwa ukarabati na hivyo kujaa udongo. Kipindi cha kiangazi kama hiki hakuna maji kabisa," alieleza Paulina Omari.

Walisema kuwa hata wanafunzi wanashindwa kufanya vizuri darasani kutokana na kushindwa kupatiwa chakula kwa wakati wazazi wao kushinda porini wakisaka maji.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Lukenge, John Urembo, alikiri kuwapo kwa hali hiyo na kwamba wananchi wake walitembea kilomita saba hadi nane kusaka maji na wengine kusubiri kisimani kwa saa 12, hivyo kushindwa kufanya shughuli nyingine.

Diwani wa Magindu, Erasto Makala, alisema kuna miundombinu ya maji ambayo imejengwa mwaka 2012-2013 lakini maji yake yanapatikana kwa shida na sasa miezi minne hayatoki kabisa.

Makala alisema lambo (bwawa) lililokuwa mbadala wa maji ya bomba kwasasa limekauka visima vilivyochimbwa vinatoa maji kwa shida na hivyo wananchi kukosa maji kutoka kwenye chanzo cha uhakika.

"Naomba serikali iingilie kati suala la maji katika kijiji hiki wananchi wanashindwa kufanya mambo mengine wanajikita kusaka maji muda wote wanaamka alfajiri na kurejea usiku huku wakiwa wameambulia maji kidogo kwa hali hii maendeleo yanadumaa," alisema.

Makala alisema wananchi hao wanapata maji safi kwa kununua dumu la lita 20 kwa Sh. 500 hadi 700 na kwa wale ambao hawana uwezo hawapati maji hayo wanaendelea kutumia maji wanayosaka kwenye visima ambayo si salama kwa kunywa.

Mhandisi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) Chalinze, Hafidhi Mketo, alikiri kuwapo kwa shida ya maji katika kijiji hicho ambayo wanaendelea kuishughulikia.

Mhandisi Mketo alisema kwa sasa uhitaji wa maji ni mita za ujazo 15,000 kwa siku na zilizopo ni 7,200 ambazo wanalazimika kusambaza kwa mgawo ili kila eneo lipate.

## Uamuzi kesi mgogoro wa ardhi Novemba 18

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu, Kanda ya Dar es Salaam imesema itatoa uamuzi Novemba 18, mwaka huu ya malalamiko yaliyowasilishwa na Amani Temba dhidi ya Monika Mjungu akitaka uamuzi wa kusikiliza kesi ya mgogoro wa ardhi kusikilizwa upande mmoja utenguliwe.

Hatua hiyo imefikiwa juzi katika mahakama hiyo iliyoketi chini ya Jaji Mfawidhi, Amiri Mruma, baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili kuhusu malalamiko yaliyowasilishwa na Temba.

Awali, wakili Benson Mpaso alidai kuwa wamewasilisha maombi hayo kwa kuwa Mtemba amekosa haki ya kumhoji mlalamikaji katika shauri namba 32/2021 lililopo Baraza la Ardhi la Wilaya ya Kinondoni.

Alidai kuwa baraza hilo liliamua kwamba shauri hilo lisikilizwa upande mmoja wa mlalamikaji na kwamba mlalamikiwa alinyimwa haki ya kumhoji mlalamikaji huyo.

"Temba alishawasilisha ombi la kuomba kutengua usikilizwaji wa upande mmoja ili apate nafasi ya kumhoji mlalamikaji, lakini lilitupwa," alidai Mpaso.

Akijibu hoja za mlalamikaji katika maombi hayo ya mapitio, Mjungu alidai kuwa tangu kesi hiyo imeanza haijawahi kutolewa hukumu na mlalamikaji huyo akashinda.

"Mtukufu Jaji, hakunyimwa haki ya kunihoji isipokuwa hajawahi kuwasilisha maombi ya aina hiyo, alipewa nafasi ya kujitetea alikataa ndipo ikaamuliwa shauri kusikilizwa upande mmoja," alidai Mjungu.

Jaji Mruma alisema amesikiliza hoja za pande zote mahakama yake itatoa uamuzi Novemba 18, mwaka huu.

Katika kesi ya msingi, Mjungu amefungua shauri hilo Baraza la Ardhi Wilaya ya Kinondoni baada ya mgogoro baada ya Temba kuvamia eneo lake Ploti namba 1121 iliyopo mtaa wa Kajima, Kata ya Makubuli, Ubungo jijini Dar es Salaam.

MAKALA MAALUM

# Teknolojia ilivyoongeza kasi upatikanaji huduma za RITA

## ●Watoto milioni saba wasajiliwa mikoa 20

Na Esther Mgidula

OFISI ya Kabidhi Wasii Mkuu, sasa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) ilianzishwa kwa madhumuni ya kutoa huduma za usajili, ufilisi na udhamini, hivyo wakati wote wakala umeendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi na kuwezesha upatikanaji wa haki na takwimu zinazotokana na usajili wa matukio muhimu ya binadamu, ufilisi na udhamini nchini.

Dhima ya wakala huo ni kusimamia haki kwa usimamizi wenye ufanisi wa kumbukumbu muhimu za maisha ya binadamu, ufilisi na udhamini ili kuchangia katika maendeleo ya taifa.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa RITA, Emmy Hudson, anasema mahitaji ya nyaraka mbalimbali za utambulisho wa wananchi yameendelea kuongezeka kwa ajili ya kuthibitisha ukweli wa taarifa wanazozitoa hasa wanapohitaji huduma nyingine katika taasisi mbalimbali nchini.

Anasema RITA ni taasisi yenye dhamana kutunza kumbukumbu za matukio muhimu ya binadamu na kutoa nyaraka muhimu na za msingi kwa wananchi ambazo ni cheti cha kuzaliwa, cheti cha kifo, cheti cha ndoa na cheti cha talaka.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu huyo anasema wananchi wamekuwa wakihitaji vyeti hivyo kwa ajili ya kupata nafasi za elimu, mikopo ya elimu ya juu, bima ya afya, ajira, bima ya maisha, huduma za kifedha, kushughulikia masuala ya mirathi na kesi za jinai katika mahakama na nyinginezo.

"Kutokana na umuhimu wake mijini na vijijini, RITA imeendelea kutekeleza mikakati na programu mbalimbali kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma zake kwa wananchi wote," anasema.

Vilevile, anatamba na mafanikio yao kwa kutambuliwa kimataifa kama moja ya taasisi zilizoleta mageuzi makubwa kwa muda mfupi katika usajili wa matukio muhimu ya binadamu na kutamkwa na Umoja wa Afrika (AU) kuwa nchi kinara katika kuongoza mageuzi hayo.

**USAJILI WA WATOTO**

Anayataja mafanikio makubwa yamepatikana, yakijumuisha mpango wa usajili wa watoto, akibainisha kuwa wakala unaendelea na utekelezaji wa Mpango wa Usajili wa Watoto wa Umri Chini ya Miaka Mitano kwa kushirikiana na wadau wa ndani na wadau wa maendeleo ambapo huduma za usajili zinatolewa bila malipo katika vituo vilivyo karibu na makazi ya wananchi, yaani ofisi za watendaji wa kata na vituo vya tiba vinavyotoa huduma ya afya ya mama na mtoto.



Sehemu ya watoto wilayani Magu mkoani Mwanza waliopata vyeti vya kuzaliwa kutoka RITA kupitia programu kutoa vyeti kwa watoto chini ya miaka mitano.

Serikali imeondoa ada ya usajili kwa watoto wa umri chini ya miaka mitano ili huduma hii iweze kuwafikia wananchi karibu na makazi yao mijini na vijijini na bila kujali hali zao za kiuchumi.

Anafafanua kuwa Mei mwaka huu, wakala umesimika mfumo wa usajili wa watoto katika mikoa ya Arusha na Manyara na zaidi ya watoto 349,018 wamesajiliwa na kupata vyeti vya kuzaliwa bila malipo baada ya serikali kuondoa ada kwa kundi hilo la kimkakati la watoto.

Pamoja na mikoa hii, idadi ya mikoa inayotekeleza mpango huu imefikia 20 na jumla ya watoto 7,004,382 wamesajiliwa, hivyo kuongeza asilimia ya watoto waliosajiliwa nchini kufikia 55 kutoka asilimia 13 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012.

Anasema matumizi ya TEHAMA kupitia simu za kiganjani yamesaidia kuongeza ufanisi katika kutuma kwa haraka taarifa za watoto waliosajiliwa kwenda katika kanzidata ya wakala, hivyo kupata takwimu sahihi na kwa wakati kwa ajili ya kupanga mipango ya maendeleo ya nchi na utoaji huduma za jamii.

"Pia matumizi ya TEHAMA yamesaidia wananchi wanaohitaji nakala za vyeti au taarifa za kumbukumbu zao, ambazo sasa zinapatikana kwa haraka tofauti na zamani," anasema.

Hudson anasema wakala upo katika maandalizi ya kuanza utekelezaji katika mikoa ya Katavi na Rukwa na kwamba Novemba mwaka huu, watoto zaidi ya 413,623 wanatarajiwa kusajiliwa na kupata vyeti vya kuzaliwa.

**USAJILI KIELEKTRONIKI**

Anasema RITA ilibuni mfumo wa E-Huduma kwa lengo la kuwafikia wananchi wengi zaidi bila wao kulazimika kufika katika Ofisi za Wakala.

"Huduma hii inamwezesha mwananchi kupata huduma ya usajili wa vizazi na vifo kwa kukamilisha sehemu kubwa ya maombi yake kielektroniki popote alipo nchini bila kujali wilaya aliyozaliwa," anasema.

Anabainisha kuwa katika kipindi cha miezi sita iliyopita huduma nyingi zimeongezwa katika mfumo huo na sasa mwananchi anaweza kuomba cheti cha kuzaliwa au kifo, kuhakiki vyeti vya vizazi na vifo kwa waombaji wa mikopo ya elimu ya juu pamoja na mahitaji mengine, kuomba nakala ya cheti na kufanya masahihisho ya cheti cha kizazi au kifo na kubadili cheti cha zamani.

"E-Huduma imeendelea kutumika kuhakiki vyeti vya kuzaliwa kwa wanafunzi wanaoomba mikopo kwa ajili ya masomo ya elimu ya juu ambapo mwanafunzi anatuma cheti kinachotakiwa kuhakikiwa na anapokea majibu yaani cheti kilichohakikiwa kwa njia ya mtandao pasipokufika Ofisi ya Wakala," anasema.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu huyo anasema tangu mfumo huo ulipoanza kutumika Juni mwaka jana, wametoa huduma kwa wananchi zaidi ya 231,978 na asilimia kubwa wakiwa wanafunzi wanaohakiki vyeti kwa ajili ya kuomba mkopo wa masomo ya elimu ya juu.

"Faida za kutumia E-huduma ni pamoja na kupunguza mlundikano wa wananchi katika Ofisi za RITA hasa katika kipindi hiki ambapo nchi yetu inaendelea na mapambano ya kuzuia kuenea kwa ugonjwa wa Uviko-19.

"Kwa upande wa serikali, mfumo huu unasaidia kuongeza uwazi, uwajibikaji, makusanyo ya maduhuli pamoja na upatikanaji wa takwimu sahihi za wananchi wanaosajiliwa na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa na vifo," anasifu.

**KUNG'ARA KIMATAIFA**

Anasema kung'ara kwa Tanzania na kuchaguliwa na AU kuongoza kampeni ya kuongeza kasi usajili wa vizazi kwa watoto barani Afrika kumetokana na mikakati mbalimbali inayofanya na wakala huo.

Anabainisha kuwa mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa mipango mbalimbali ya wakala yameiwezesha Tanzania kutambulika kimataifa kama moja ya nchi zilizoleta maboresho ya haraka ya mfumo wa usajili kwa muda mfupi.

AU imeichagua Tanzania kuwa miongoni mwa nchi tano za Bara la Afrika zitakazoongoza kampeni ya kuongeza kasi ya usajili wa vizazi kwa watoto barani Afrika inayojulikana kama 'Bila kuwa na Jina; Utambulisho wa Kisheria kwa Kila Mtoto; Upatikanaji wa Haki kwa Kila Mtoto', ambayo inaendeshwa kwa ushirikiano na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Umoja wa Afrika (AU) na Center for Excellence ya Canada.



Emmy Hudson

Anafafanua kuwa Tanzania inatekeleza jukumu hilo katika nchi za Ukanda wa Mashariki wa Bara la Afrika na imechaguliwa kutokana na mafanikio iliyoyapata miaka ya karibuni katika kuongeza kasi ya usajili wa matukio muhimu ya binadamu hasa usajili wa vizazi kwa watoto.

"Sababu nyingine zilizoainishwa ni pamoja na nchi kuwa na utashi wa kisiasa katika masuala ya usajili wa vizazi na kutekeleza kikamilifu kanuni muhimu zinazounga mkono kampeni hii," alisema.

Aliongeza kuwa mpango wa usajili wa watoto umeenezwa katika mikoa 20 ambayo mpaka sasa inautekeleza na umekuwa wa mfano wa kuigwa na nchi nyingi barani Afrika.

"Mojawapo ya nchi zilizokuja kujifunza nchini ni Uganda ambayo maofisa wake walikuja kabla ya mlipuko wa ugonjwa wa Uviko-19. Nchi nyingi kutokana na changamoto ya Uviko-19 sasa wanajifunza kwa njia ya mtandao.

"Aidha, wakala unatekeleza Mpango wa Usajili wa Watoto wa Umri kati ya Miaka 5-17 ambapo wanafunzi wanasajiliwa na kupata vyeti vya kuzaliwa katika shule wanazosoma.

"Mpaka sasa wanafunzi 384,413 wamesajiliwa na kupata vyeti vya kuzaliwa katika wilaya 19. Wakala upo katika maandalizi ya kufanya zoezi hilo katika Wilaya za Arumeru na Arusha."

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu huyo anasema RITA ni moja ya taasisi ambazo zimejiunga katika vituo vya huduma pamoja katika ofisi za Shirika la Posta Tanzania.

Anasema huduma zinaendelea kutolewa katika maeneo hayo na kwa kuanzia, huduma hizo zinatolewa katika majiji ya Dodoma na Dar es Salaam.

Anasema kuanzishwa kwa vituo hivi ni mkakati wa serikali kuweka mazingira rahisi na wezeshi kwa wananchi kupata huduma zote za serikali ndani ya eneo moja kwa muda mfupi.

Huduma zinazotolewa na RITA katika vituo hivyo ni pamoja na usajili wa vizazi na vifo kwa kutumia njia ya mtandao kupitia mfumo wa E-Huduma.

"Tunawashauri wananchi kutumia fursa ya huduma pamoja ili kujipatia huduma mbalimbali katika sehemu moja na kwa wakati mmoja," anahitimisha.

# KILI MARATHON YAZINDULIWA RASMI, ZAWADI ZAONGEZWA

**Na Mwandishi Wetu**

MBIO za Kilimanjaro Premium Lager Marathon maarufu Kili marathon kwa mwaka 2022, zimezinduliwa rasmi jana jijini Dar es Salaam, ikiwa ni msimu wake wa 20 tangu zilipoanzishwa.

**Mbio hizo zimepangwa kufanyika Februari 27, mwakani mkoani Kilimanjaro na uzinduzi wake ulishirikisha wadau mbalimbali wa riadha kutoka ndani na nje ya Tanzania.**

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, mgeni rasmi katika hafla hiyo ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) Jaji, Thomas Mihayo (mstaafu) aliwapongeza waandaaji na wadhamini wa mashindano hayo kwa ushirikiano wao ambao umezifanya mbio hizo kuwa maarufu ndani na nje ya nchi.

Mihayo alisema mbio za Kilimanjaro zimekuwa na mchango mkubwa katika kukuza sekta ya utalii hapa nchini kupitia utalii wa michezo, jambo ambalo linaunga mkono juhudi za serikali katika utekelezaji wa sera za utalii na michezo.

"Nichukue fursa hii muhimu kuwapongeza wadhamini wote wakiongozwa na mdhamini mkuu Kilimanjaro Premium Lager, Tigo ambao ni wadhamini wa Half Marathon) na Grand Malt ambao ni wadhamini wa mbio za kujifurahisha za kilomita tano," alisema Mihayo na kuongeza bila wadhamini hao mashindano hayo yasingefana.

Aliwataka wafanyabiashara kutumia fursa ya mbio hizo kukuza biashara zao pamoja na kutoa huduma bora huku akiwashauri washiriki wote kuhakikisha wanatumia msimu huo kwenda kutembelea vivutio mbalimbali vya utalii.

Naye Mkurugenzi wa Michezo katika Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo, Yusuf Singo alitoa wito kwa waandaaji wengine kuhakikisha wanaiga mfano wa Kilimanjaro marathon ambao huzingatia mwongozo wa Shirikisho la Riadha Duniani (IAAF) na wa Chama cha Riadha Tanzania (RT), hatua ambazo zimewavutia wadhamini mbalimbali.

Naye Meneja wa bia ya Kilimanjaro na chapa Grand Malt, Irene Mutiganzi, alisema mashindano yajayo yatakuwa ya hatua muhimu kutokana na kampuni yake kuwa mdhamini mkuu wa mbio hizo kwa muda wa miaka 20.

"Tunatarajia kuyafanya mashindano hayo ya maadhimisho ya miaka 20 kwa namna ya pekee, kwani ni ya kihistoria kutokana na ukweli ni moja ya udhamini mrefu kupitia chapa ya Kilimanjaro Premium Lager na ambayo imeifanya chapa hiyo kukua mwaka hadi mwaka", alisema Mutiganzi.

Alisema kampuni ya TBL kupitia bia yake ya Kilimanjaro Premium Lager imejiandaa vyema kwa maadhimisho ya Miaka 20 ya mashindano hayo maarufu.

"Tumetenga zawadi za kifedha zenye thamani ya jumla ya Sh. milioni 25, ambapo washindi wa kwanza katika mbio za 42, kwa wanawake na wanaume watapata zawadi ya Sh. milioni nne kila mmoja," alisema na kuongeza katika mbio hizo za kilometa 42 kutakuwa na motisha ya ziada ya Sh. milioni 1.5 kwa kila Mtanzania atakayemaliza wa kwanza upande wa wanaume na wanawake.

Aliwataka wadau kujiandikisha mapema wakati zoezi hilo litakapoanza rasmi kuanzia Oktoba 17, mwaka huu hadi Januari 7 mwakani kupitia anuani ya mtandano www.kilimanjaromarathon.com na kupitia Tigo Pesa kwa kupiga * 149 * 20.

Aliongeza kwa kuwataka washiriki wa mbio za kujifurahisha za kilomita tano kujiandikisha mapema kwani nambari za wanaotarajiwa kushiriki kipengele hicho zinatarajiwa kupunguzwa.

Meneja wa Tigo, Anna Loya alisema kampuni yao imekuwa mstari wa mbele kudhamini mbio za Tigo Kili Half marathon kwa miaka saba sasa na kwamba kuwapo kwao kuendelea kuchangia kukuza vipaji vya wanariadha na sekta ya michezo kwa ujumla hapa nchini.

"Nichukue fursa hii kuwahimiza wanaotarajia kushiriki mbio za Tigo Half Marathon kwa mwaka 2022, kujiandikisha mapema kupitia Tigo Pesa ili kuepuka usumbufu wa kung'ang'ania dakika za mwisho," Loya alishauri.

Mbio hizo zimeandaliwa na Kampuni ya Kilimanjaro Limited na kuratibiwa na Kampuni ya Executive Solutions Limited.

## Mnyamani yang'ara bonanza la VVU

**Na Mwandishi Wetu**

MRATIBU wa Kudhibiti Ukimwi katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Barnabas Kisai, amesema mashindano mbalimbali yaliyofanyika katika Kata za Buguruni, Vingunguti, Mnyamani, Tabata na Kipawa yamesaidia kufikisha elimu ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa Ukimwi kwa vijana kwenye eneo hilo.

Mashindano hayo yaliyofanyika kwenye Uwanja wa Sinai Vingunguti yaliandaliwa na Shirika lisilo la Kiserikali la CAFLO ambalo linatekeleza mradi wa kudhibiti maambukizi ya VVU katika kata hizo. Kisai alisema vijana wanaoshiriki michezo hiyo wamepata elimu na mafunzo mbalimbali yanayohusiana na kujikinga na ugonjwa huo.

Timu ya Peace and Love kutoka Mnyamani iliibuka mshindi katika mchezo wa mstari kati wakati Majumba Sita Queens ya Kipawa ilinyakua ubingwa wa mpira wa pete na kwa upande wa soka, Mnyamani Youth Initiative iliibuka mshindi na washindi wote kuzawadiwa mbuzi.

Pia kulikuwa na mashindano ya kukimbia kwa viroba, kuvuta kamba, kukimbiza kuku na kuimba.

## Biashara Utd majaribuni

**Na Saada Akida**

WAWAKILISHI wa Tanzania katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, Biashara United leo wanatarajia kuwavaa Al Alhly Tripoli kutoka Libya kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam.

Kocha Mkuu wa Biashara United, Patrick Odhiambo, alisema mechi hiyo itakuwa ni yenye ushindani na anawafahamu vyema wapinzani wao ambao aliwahi kukutana nao alipokuwa na kikosi cha Gor Mahia ya Kenya.

Odhiambo alisema maandalizi ya mchezo huo yamekamilika na wachezaji wote wako tayari kwa mapambano huku wakijipanga kuongeza umakini hasa katika safu ya ushambuliaji.

Naye Mwenyekiti wa Biashara United, Suleiman Mataso, amesema anaamini kikosi chake kitaendeleza kasi waliyoianza kwenye mashindano hayo ya kimataifa ingawa alikiri wanakutana na changamoto mbalimbali.

Biashara United ilisonga mbele katika mashindano hayo baada ya kuwaondoka FC Dikhil ya Djibouti kwa jumla ya mabao 3-0 wakati Al Ahly Tripol iliwachapa Hay Al Wad ya Sudan magoli 4-0.



Wachezaji wa Biashara United wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Al- Ahly Tripol kutoka Libya utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Geita Gold vinara wa kadi za njano

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara raundi ya tatu ikitarajia kuendelea kesho kwenye viwanja mbalimbali nchini, timu ya Geita Gold FC ndiyo inayoongoza kwa wachezaji wake kucheza rafu na kufanya makosa ya utovu wa nidhamu.

Kwa mujibu wa takwimu za Ligi Kuu, Geita Gold iliyoanza kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, ina kadi nne za njano walizoonyeshwa wachezaji wake, huku jumla ya kadi 26 zikitolewa mpaka sasa, kati ya hizo, mbili zikiwa nyekundu.

Wachezaji wa Geita Gold walioonyeshwa kadi za njano ni Hamisi Kadikilo, Yusuph Kagoma, Daniel Lyanga na Dereck Mussa.

Takwimu zinaonyesha wachezaji wawili ambao mpaka kufikia raundi ya pili walikuwa wametwangwa kadi nyekundu ni Ismail Gambo wa KMC, lakini ikiwa ni njano mbili ambayo sawa na nyekundu moja, huku Anuary Jabir wa Dodoma Jiji aliyeonyeshwa nyekundu ya moja kwa moja, kwenye mechi ya kati ya timu hiyo dhidi ya Simba.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### WERNER ANUKIA NEWCASTLE

WAMILIKI wapya wa Newcastle wameripotiwa wanataka kumsajili mshambuliaji wa Chelsea, Timo Werner, 25. ***(Bild)***

#### FOFANA AINGIA SOKONI

NEWCASTLE wamewasiliana na wawakilishi wa nyota wa Leicester City, Wesley Fofana kuhusu uwezekano wa uhamisho katika dirisha la Januari, mwakani. ***(RMC Sport)***

#### RABIOT KITAELEWEKA

KIUNGO wa kati wa Juventus na Ufaransa, Adrien Rabiot, 26, amehusishwa na uhamisho wa Newcastle, huku klabu hiyo ya Serie A ikiwa tayari kumuuza mchezaji huyo ifikapo Januari. ***(Calciomercato)***

#### TCHOUAMENI RASMI KUUZWA

KLABU ya Monaco imeweka dau la euro milioni 60 kwa Aurelien Tchouameni, 20, huku Real Madrid, Manchester City, Chelsea na Liverpool zikionyesha nia ya kumtaka mchezaji huyo. ***(Marca)***

#### COUTINHO NJIA MOJA

BARCELONA wako tayari kumwachia, Philip Coutinho, 29, katika kipindi cha dirisha la uhamisho la Januari, huku Liverpool ikijiandaa kumrejesha tena mchezaji huyo. ***(El Chiringuito TV, via Express)***

#### RODGERS NEEMA YANUKIA

KOCHA wa Leicester City, Brendan Rodgers ndiye mtu wa kwanza anayefikiriwa kuchukuliwa na wamiliki wapya wa klabu ya Newcastle iwapo wataamua kumfuta kazi, Steve Bruce. ***(Sky Italy via Mirror)***

#### MADRID YAMTAKA RUDIGER

REAL Madrid wanania ya kumsajili mlinzi wa Chelsea, Antonio Rudiger, 28. Mkataba wa mchezaji huyo unamalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Marca)***

#### FODEN AIKATAA CITY

PHIL Foden amesitisha mpango wake wa kusaini mkataba na Manchester City wenye thamani ya karibu pauni milioni 50. ***(Mirror)***

#### LANG AKARIBIA ARSENAL

ARSENAL wanajiandaa kwa dau la euro milioni 30 kwa ajili ya winga wa klabu ya Club Bruges, Noa Lang, 22, ambaye ni raia wa Uholanzi. ***(Voetbal24)***

#### KOUNDE AWINDWA EPL

MANCHESTER United wanaweza kufufua juhudi zao za kutaka kumsajili, Jules Kounde ambaye bado analengwa na Chelsea. ***(Fichajes, via FourFourTwo)***

#### BARCA, PEDRI MAMBO SAFI

BARCELONA wamepiga hatua katika mazungumzo yao na kiungo wa kati wa Hispania, Pedri, 18 kuhusu mkataba mpya, na kiungo huyo yuko tayari kukubali mkataba ambao utaendelea hadi mwaka 2026. ***(Goal)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# LINGARD ATAKIWA BARCELONA, AC MILAN

### ●●● Ni baada ya mchezaji huyo kuonyesha nia ya kutaka kuondoka...

**MANCHESTER,** England

JESSE Lingard anawaniwa na Barcelona na AC Milan wakati mkataba wake ukikaribia kufikia mwisho pale Manchester United, kwa mujibu wa vyanzo vya ESPN.

Lingard ameingia katika mwaka wake wa mwisho katika mkataba na klabu hiyo inayotumia Uwanja wa Old Trafford, atakuwa na uwezo wa kuanza mazungumzo na timu yoyote kuanzia Januari Mosi, kuelekea kuondoka kama mchezaji huru kipindi cha majira ya joto kinachokuja.

Barcelona na AC Milan ni miongoni mwa klabu zinazomfuatilia, na Lingard yupo wazi kuhamia Hispania au Italia wakati akitaka kuendeleza kipaji chake.

**Kwa hiyo nyota huyo wa England ana nafasi ya kuhamia klabu nyingine kama mchezaji huru kipindi cha majira ya joto kinachokuja.**

Lingard tayari amekataa ofa ya mkataba mpya kutoka United kwa madai hana uhakika wa kupata nafasi ya kucheza mara kwa mara katika kikosi hicho ili aweze kurudishwa katika Timu ya Taifa chini ya Kocha, Gareth Southgate kuelekea fainali za Kombe la Dunia 2022.

Na hadi sasa Manchester United hawajatoa ofa nyingine yoyote kwa mchezaji huyo.

Lingard amefunga mabao mawili kwenye mechi za Ligi Kuu England msimu huu likiwamo la ushindi katika dakika za majeruhi dhidi ya West Ham United, mechi iliyochezwa Septemba, mwaka huu.

MECHI KALI
HOME
PARIS ST GERMAIN
1.35 | 5.11 | 7.66
ANGERS
AWAY

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 576

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# MAN CITY YAKOMAA NA HAALAND

**MANCHESTER,** England

WAKALA wa Erling Haaland, Mino Raiola anatarajiwa kuwa na mazungumzo na mabosi wa klabu ya Manchester City kuhusu uwezekano wa uhamisho wa mshambuliaji huyo wa Borussia Dortmund ifikapo Januari 2022.

Mkataba wa Haaland mwenye umri wa miaka 21 kwenye klabu ya Dortmund utafikia kikomo mwaka 2024.

Lakini una kipengele cha kumnunua kwa pauni milioni 64 kinachoanza kutumika mwaka 2022.

Inaaminika kuwa City inamwona raia huyo wa Norway kama lengo lao kuu la usajili baada ya msimu uliopita kushindwa kupata saini ya Harry Kane.

Baba wa Haaland, Alf-Inge aliwahi kucheza City kati ya mwaka 2000 na 2003 na anaonekana kuwa mtu mwenye ushawishi wa uhamisho wa mchezaji huyo.

Manchester United, Real Madrid, Barcelona pia zimekuwa zikitajwa kuwania huduma ya mchezaji huyo.



# Foden apewa miaka sita Manchester City

**MANCHESTER,** England

PHIL Foden anatarajiwa kusaini mkataba mpya wa muda mrefu wa miaka sita na Manchester City, kwa mujibu wa ESPN.

Kiungo huyo hivi sasa anaonekana kuwa mchezaji muhimu zaidi kwa Kocha, Pep Guardiola.

Kwa mujibu wa vyanzo vya ESPN Manchester City inatarajia kutangaza kumpa mkataba mpya mchezaji huyo mara tu kila kitu kitakapofikiwa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 amekuwa nyota muhimu zaidi kwa kikosi hicho tangu alipopandishwa kutoka kwenye akademi ya klabu hiyo.

Amecheza mechi 50, akifunga mabao 16, wakati Manchester City iliposhinda taji la Ligi Kuu England na kufika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita.

Kiwango chake cha msimu uliopita kilimfanya apate nafasi ya kuitwa kwenye kikosi cha Kocha wa Timu ya Taifa ya England, Gareth Southgate na alikuwa sehemu ya timu hiyo kwenye michuano ya Euro 2020.

Alilazimika kukosa fainali ya michuano hiyo dhidi ya Italia baada ya kuumia na alikosa mechi nne za kwanza za Manchester City msimu huu.

## HABARI MICHEZO

# ,086,780

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

**BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13**

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 16/10/21 | 17:00 | Southampton vs Leeds | 2.40 | 3.52 | 2.82 |
| 02. 16/10/21 | 17:00 | Blackburn vs Coventry | 2.81 | 3.11 | 2.52 |
| 03. 16/10/21 | 17:00 | Millwall vs Luton Town | 2.30 | 3.20 | 3.06 |
| 04. 16/10/21 | 17:00 | Girona vs Huesca | 2.44 | 2.87 | 3.16 |
| 05. 16/10/21 | 19:15 | Las Palmas UD vs Tenerife | 2.51 | 2.95 | 2.95 |
| 06. 16/10/21 | 19:30 | Levante vs Getafe | 2.56 | 2.91 | 3.11 |
| 07. 16/10/21 | 21:30 | Malaga vs Zaragoza | 2.53 | 2.97 | 2.92 |
| 08. 17/10/21 | 13:30 | Cagliari vs Sampdoria | 2.72 | 3.37 | 2.56 |
| 09. 17/10/21 | 14:00 | Swansea vs Cardiff | 2.44 | 3.06 | 2.96 |
| 10. 17/10/21 | 16:00 | Everton vs West Ham | 2.38 | 3.42 | 2.92 |
| 11. 17/10/21 | 16:00 | Bordeaux vs Nantes | 2.78 | 3.13 | 2.59 |
| 12. 17/10/21 | 16:00 | Udinese vs Bologna | 2.36 | 3.35 | 3.00 |
| 13.17/10/21 | 17:00 | Leganes vs Valladolid | 2.46 | 2.97 | 3.02 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### IJUMAA - 15 - OKTOBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 1324 | Shabab Alsamu vs Hilal Al-Quds | 3.58 | 3.34 | 1.94 |
| 17:00 | 4309 | Shakhtar Donetsk vs Zorya Lugansk | 1.44 | 4.36 | 5.81 |
| 18:00 | 1027 | Liptovsky Mikulas vs AS Trencin | 3.15 | 3.63 | 1.99 |
| 18:00 | 2079 | Inter Zapresic vs Orijent Rijeka | 3.58 | 3.14 | 2.01 |
| 18:00 | 2088 | Zbrojovka Brno vs Vyskov | 1.28 | 5.40 | 7.71 |
| 19:00 | 2405 | Hrvatski Dragovoljac vs Lokomotiva Zagreb | 4.85 | 3.97 | 1.57 |
| 19:30 | 2424 | Floridsdorfer AC vs Vorwarts Steyr | 1.58 | 4.07 | 4.65 |
| 19:30 | 2893 | FC Liefering vs FC Juniors OO | 1.27 | 5.60 | 7.92 |
| 19:30 | 3371 | SKN St Polten vs Liebherr Gak | 2.13 | 3.49 | 2.95 |
| 19:30 | 3843 | Austria Lustenau vs Kapfenberg | 1.42 | 4.55 | 5.81 |
| 19:30 | 4453 | Hannover vs Schalke 04 | 2.62 | 3.36 | 2.52 |
| 20:00 | 2329 | Fremad Amager vs FC Fredericia | 3.77 | 3.62 | 1.81 |
| 20:00 | 2796 | Viborg FF vs Silkeborg | 2.17 | 3.64 | 2.95 |
| 20:00 | 3066 | Viktoria Berlin vs Osnabruck | 2.61 | 3.25 | 2.56 |
| 20:00 | 3920 | Skive IK vs Aarhus Fremad | 2.81 | 3.49 | 2.21 |
| 20:00 | 4301 | Basaksehir vs Besiktas | 2.95 | 3.34 | 2.29 |
| 20:30 | 3103 | Gaz Metan Medias vs Dinamo Bucuresti | 2.06 | 3.10 | 3.69 |
| 21:00 | 2843 | Telstar vs FC Volendam | 4.57 | 4.18 | 1.59 |
| 21:00 | 2977 | De Graafschap vs FC Eindhoven | 1.30 | 5.27 | 8.00 |
| 21:00 | 3266 | MTK Budapest vs Puskas Akademia | 2.76 | 3.44 | 2.26 |
| 21:00 | 3342 | Helmond Sport vs ADO Den Haag | 4.00 | 3.85 | 1.74 |
| 21:00 | 3501 | FC Oss vs Emmen | 2.97 | 3.36 | 2.22 |
| 21:00 | 3927 | NAC Breda vs Jong AZ Alkmaar | 1.58 | 4.12 | 4.80 |
| 21:00 | 4117 | Roda Kerkrade vs Jong PSV | 1.50 | 4.40 | 5.28 |
| 21:00 | 4762 | Maastricht vs Dordrecht | 1.86 | 3.86 | 3.47 |
| 21:00 | 4931 | Den Bosch vs Almere City | 3.87 | 3.91 | 1.75 |
| 21:00 | 5672 | SBV Excelsior vs VVV Venlo | 1.97 | 3.62 | 3.33 |
| 21:30 | 1806 | Neuchatel Xamax vs FC Vaduz | 2.00 | 3.83 | 3.00 |
| 21:30 | 2185 | FC Stade LS Ouchy vs FC Aarau | 2.10 | 3.98 | 2.72 |
| 21:30 | 3465 | Hoffenheim vs FC Koln | 2.00 | 3.83 | 3.29 |
| 21:30 | 3500 | Korona Kielce vs Widzew Lodz | 2.12 | 3.19 | 3.24 |
| 21:30 | 4599 | FC Thun vs FC Winterthur | 2.00 | 3.62 | 3.14 |
| 21:45 | 1373 | Waterford Utd vs Finn Harps | 2.66 | 3.10 | 2.52 |
| 21:45 | 1602 | Treaty United vs Athlone Town | 2.01 | 3.65 | 3.50 |
| 21:45 | 1854 | Burton vs Morecambe | 1.91 | 3.36 | 3.95 |
| 21:45 | 2256 | Derry City vs St Patricks | 2.96 | 3.15 | 2.28 |
| 21:45 | 2361 | Galway United vs Wexford Youths | 1.29 | 5.22 | 7.93 |
| 21:45 | 2719 | Drogheda Utd vs Longford Town | 1.36 | 4.63 | 6.95 |
| 21:45 | 2857 | UCD Dublin vs Cork City | 1.73 | 3.87 | 3.87 |
| 21:45 | 3330 | Edinburgh City vs Kelty Hearts FC | 4.83 | 3.77 | 1.61 |
| 21:45 | 3411 | Hamilton vs Partick Thisle | 2.94 | 3.24 | 2.29 |
| 21:45 | 3472 | Bray Wanderers vs Cabinteely | 1.34 | 5.01 | 6.74 |
| 21:45 | 3751 | Cobh Ramblers vs Shelbourne | 10.68 | 5.63 | 1.21 |
| 21:45 | 3911 | Brugge vs Kortrijk | 1.23 | 5.90 | 10.82 |
| 21:45 | 4719 | Bohemians FC vs Dundalk FC | 1.82 | 3.64 | 3.68 |
| 22:00 | 1580 | Paris St Germain vs Angers | 1.35 | 5.11 | 7.66 |
| 22:00 | 3759 | Shamrock Rovers vs Sligo Rovers | 1.57 | 3.64 | 5.43 |
| 22:00 | 5236 | West Bromwich vs Birmingham | 1.58 | 3.94 | 5.33 |
| 22:00 | 5408 | Eibar vs Almeria | 2.32 | 3.16 | 3.06 |
| 22:00 | 5924 | CD Palestino vs O Higgins | 1.67 | 3.58 | 4.65 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# AGUERO 'FITI' KUONGEZA UHAI BARCA




**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA wanaweza kumtumia hivi karibuni Sergio Aguero baada ya fowadi huyo kurudi kwenye mazoezi Jumatano na kuonekana kuwa fiti.

Aguero alijiunga na Barca kama mchezaji huru baada ya mkataba wake kule Manchester City kumalizika mwishoni mwa msimu uliopita.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 aliisaidia Argentina kushinda taji la Copa America, lakini aliumia kigimbi kabla ya kuanza kwa msimu huu 2021-22 na kumfanya akose wiki za kwanza za msimu huu. Kocha wa Barca ambaye yupo kwenye presha kubwa, Ronald Koeman atakuwa anahitaji zaidi msaada wa mchezaji huyo.

Blaugrana hao wapo nafasi ya tisa kwenye msimamo wa LaLiga baada ya kufungwa mabao 2-0 na Atletico Madrid katika mechi yao ya mwisho, huku pia wakipoteza mechi zote mbili za mwanzo za makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Na sasa Aguero alirudi kwenye mazoezi wakati wa mapumziko ya kupisha mechi za kimataifa na alicheza mchezo wa mazoezi dhidi ya UE Cornella.

Inasubiriwa kuona kama Aguero atakuwa fiti kucheza mchezo wa Jumapili dhidi ya Valencia, wakati Barca wakipambana kurudi kwenye kiwango chao.



# *Liverpool yatangaza kumwania Dembele*

**LIVERPOOL,** England

IMERIPOTIWA kuwa Liverpool imeanza majadiliano ya kumsajili mshambuliaji wa Barcelona, Ousmane Dembele kwa uhamisho uhuru msimu ujao.

Mkataba wa winga huyo pale Nou Camp unafikia kikomo mwisho wa msimu huu na wawakilishi wake wanasemekana tayari wanasikiliza nia za klabu zinazotaka kumsajili.

Kwa mujibu wa gazeti la Mundo Deportivo la Hispania, Liverpool ina nia ya dhati kumleta Dembele Anfield na inamwona kama mchezaji muhimu katika kujenga upya safu ya ushambuliaji ya timu hiyo.

Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp inasemakana anamhitaji Dembele mwenye umri wa miaka 24 na Mkurugenzi wa Michezo wa klabu hiyo, Michael Edwards tayari ameripotiwa kufanya mawasiliano na mwakilishi wa Dembele, Moussa Sissoko.

Liverpool haiwezi kujadiliana rasmi na Dembele hadi Januari Mosi, mwakani atakapofikia miezi sita ya mwisho ya mkataba

# Michezo

Ijumaa Oktoba 15, 2021

Nipashe




Lingard atakiwa Barca, AC Milan UKURASA 21




Mwenyekiti wa Bodi ya Utalii Nchini (TTB), Jaji mstaafu Thomas Mihayo (katikati), akiongoza kukata keki kwa ajili ya uzinduzi wa mbio za Kilimanjaro Marathon 2022 uliofanyika jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo, Yusuf Singo, Meneja wa Chapa ya Tigo, Anna Loya na kulia ni Katibu wa Chama cha Riadha Dar es Salaam (DAAA), Rahim Kassim. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Azam FC yatamba kuimaliza Pyramids

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, amesema kikosi chake kiko imara na kamili kuwakabili Pyramids katika mechi ya hatua ya kwanza ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Vivier alisema wachezaji wake wameimarika na wako tayari kupambana kusaka matokeo mazuri. Vivier alisema wamewafuatilia kwa umakini wapinzani wao na kufahamu ubora na mapungufu waliyonayo na kuelekea mchezo huo, wamejipanga kuwashangaza.

"Mchezo wa soka una matokeo matatu kushinda, kushindwa na kutoka sare, tunatambua mechi haitakuwa rahisi na tumejipanga vizuri kutafuta ushindi katika uwanja wetu wa nyumbani," alisema Vivier.

Aliongeza ni lazima wachezaji wake wapambane kutafuta matokeo mazuri iwe nyumbani au ugenini na kwa kufanya hivyo, watajiweka kwenye nafasi ya kusonga mbele katika michuano hiyo.

Alisema endapo watapata matokeo hapa nyumbani, watajiweka kwenye nafasi nzuri wao kuelekea mchezo wa marudiano utakaochezwa nchini Misri.

"Tupo tayari kwa ajili ya ushindani, baada ya kushinda mechi mbili za awali, kuna vitu mbalimbali tulijifunza, vimetuimarisha, tunajua mechi itakuwa ngumu kwetu na hata kwao Pyramids, matarajio yetu ni makubwa," Ofisa Habari wa Azam FC, Zakaria Thabit aliliambia gazeti hili.

# Yanga yajiweka mguu sawa

### Nabi asema wanahitaji kushinda kila mechi...

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha wanaendelea kupata matokeo mazuri kwenye mechi zake za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, kikosi cha Yanga kimewaandalia wachezaji wake programu maalumu ya mazoezi ya viungo kwa malengo ya kuimarisha stamina zao, imeelezwa.

**Yanga inajiandaa kuwafuata wenyeji KMC FC katika mechi ya raundi ya tatu itakayochezwa Oktoba 19, mwaka huu kwenye Uwanja wa Majimaji ulioko Songea mkoani Ruvuma.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi (pichani) alisema anahitaji kuona wachezaji wake wanakuwa imara zaidi ili kukabiliana vyema na ushindani ulioko kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.




Nabi alisema anahitaji kupata matokeo mazuri katika kila mechi na ili kufikia malengo hayo, analazimika kuona wachezaji wake wote wanakuwa imara na tayari kwa mapambano. Kocha huyo alisema mechi zote za ligi hiyo ni muhimu kwa sababu zinakupatia pointi na mwisho wa msimu ndio bingwa hupatikana.

"Tunafanya mazoezi ya aina mbalimbali, kwa sasa tumezingatia zaidi kujenga stamina, wachezaji wanatakiwa kuwa imara, ligi ni safari ndefu, wanatakiwa wawe katika kiwango cha juu cha kushindana kuanzia mwanzo hadi mwisho wa msimu," alisema Nabi.

Aliongeza wanahitaji kuongeza umakini na kucheza kwa tahadhari katika mechi yao inayofuata kwa sababu watakuwa kwenye mazingira tofauti na waliyoyazoea.

"KMC ni moja ya timu ambazo wachezaji wake wanatumia nguvu, ninajua namna ambavyo tutawakabili, naamini tutapata kile ambacho tunakihitaji kama timu," Nabi alisema.

Aliongeza kurejea kwa wachezaji wake waliokuwa kwenye timu za taifa mbalimbali kutawanufaisha kwa sababu huko pia walikuwa kwenye mazoezi magumu na yenye kuhitaji kuzalisha matokeo chanya.

"Tunahitaji ushindi katika mechi hiyo ili kutuweka kwenye nafasi nzuri, tukipata matokeo mazuri yatatuweka kwenye nafasi nzuri ya kuelekea katika maandalizi ya kuwakabili Azam, mechi zote zinahitaji kuwa na kikosi imara," Nabi aliongeza.

Kikosi cha KMC kinaondoka leo mapema kuelekea Songea tayari kuwasubiri wageni wao.

Yanga imeshinda mechi zake mbili za kwanza ambapo ilianza kwa kuwafunga Kagera Sugar bao 1-0 na ilipata matokeo kama hayo ilipowakaribisha Geita Gold FC kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >